# Mwongozo wa mwalimu

## Wakati wa biblia Kiwango 1 na 2

Msururu A
Masomo 7 - 12

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)

**Misheni yetu**

Kutunga mafundisho ya Biblia kwa walimu ili wafundishe ukweli wa Yesu Kristo kwa kizazi kinachokuja katika dunia yote.

**Maono yetu**

Kufikia kizazi kinachokuja na ufahamu wetu wote katika lugha zao kwa kuendeleza na kusaidia shirika la kimataifa la washiriki waliojitolea.

## HABARI KWA JUMLA

**Kazi inayofanywa na Bible Educational Service:**

Kazi ya mafundisho ya kibiblia (Bible Educational service) inachapisha katika kingereza mafundisho ya Biblia “Bibletime”', “New Life” na “Gleaner”. Inasaidia vituo vya usambazaji wa mafundisho hii na kila shirika ya namna hiyo inayozitumia katika Uingerezana na pahali pengine duniani, kwa njia ya kuwatembelea, kuwashauri, na wakati wa kuwafundisha. Katika inchi mbalimbali, Bes iliendeleza pia ushirikiano na vikundi nyingi vinavyofanya kazi ya utafsiri, muundo, uchapishaji na usambazaji wa mafundisho. Kila mara inapewa bure kwa wote.

Mafundisho “wakati wa biblia” ilianza pale Irland tangu miaka zaidi ya 50. BES iko na hati miliki ya mafundisho katika kiingereza vilevile katika lugha zote zingine. Sehemu kubwa ya mafundisho hii imechapishwa katika muundo wa A4 na inatumiwa kama mafundisho kwa mfano wa barua katika inchi nyingi zinazozungumza Kiingereza. Kama inajazwa na watoto, masomo inarudishwa, baada ya kila wiki ine, katika kituo kimoja ili ipewe pointi (Bible school Center). Tangu muda mfupi, mafundisho imechapishwa pia katika vitabu vya muundo wa A5, vilivyo na mafundisho ya miezi sita, kupitia Revival Movement katika Irland ya kaskazini. Hii iliwezesha kabisa utumizi wake katika ma kanisa na shule, zaidi katika eneo ambapo kazi ya posta haiko tena.

Mafundisho ya BES inapatana pia vema na utumizi wa kibinafsi nyumbani ao katika kundi, ikiwa ndani ya ma kanisa ao ndani ya ma shule. Programu iliyotungwa inawezesha watoto na vijana kuendelea kujifunza Biblia muda wa zaidi ya miaka kumi. Viwango tano vya masomo vinapatikana sasa katika kingereza (miaka 3 - 4, miaka 5 – 7, miaka 8 - 10, miaka 11 – 13, miaka 14 – 16). Kwa kila mmoja wao, programu inachukua miaka tatu. Mtoto ao kijana anaweza kujifunza viwango tofauti kulingana na uwezaji wake kibinafsi. “Wakati wa biblia” inaleta kwa watoto na vijana nafasi kwa kujifunza Neno la Mungu, kujifunza hadisi za Biblia na kuelewa maana ya injili katika maisha yao wenyewe.

Mafundisho inayopatikana katika ufaransa inaweza kuchapishwa kutoka tovu – www.besweb.com – ao kwa kumuomba katibu wa kimataifa. Inapatikana pia kwa lugha zingine katika tovu. Pia kuna vitabu vingine ambavyo vinaweza kuwa vya muhimu kwa inchi mpya ao maeneo inayotaka kuanzisha kituo cha BES.

## Anuani ya kufaa:

**UK (Northern Ireland) Office(ghala za masomo zote)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Phone: 0286 632 2462

Site web: www.besweb.com
Email: info@besweb.com

## MWONGOZO WA MWALIMU

Katika mwanzo, mafundisho ya “Wakati wa Biblia” ilitolewa kwa mfano wa mafundisho kwa njia za barua kwa ushirikiano na kituo kimoja cha “shule ya Biblia kwa njia ya posta”. Lakini, zaidi na zaidi mafundisho hii inasomwa pahali ambapo kazi ya posta siyo ya kuaminika, hasa katika shule na ma kanisa katika Afrika, India na pahali pengine. Mwongozo wa mwalimu uko pale kwa kusaidia wale wanaotumia mafundisho katika mazingiza kama haya. Kitabu hiki kinatungwa juu ya kuwa mwongozo wa kiwango 1 na 2, ambavyo vinakusudiwa watoto kutoka umri wa miaka 5 hadi 10.

Maelezo ya mwongozo huu yanafuata maandiko ya Biblia ambayo ni namna moja na ile iliyo katika mafundisho yenyewe. Mafundisho, na maelezo, imetungwa mu namna ya somo moja kwa wiki. Kwa hiyo, masomo katika Aprili inaambatana na Pasaka na masomo katika Desemba inaambatana na Krismasi.

Kulingana na pahali, ao masomo kwa wiki katika muundo wa A4, ao vitabu vya muundo wa A5 ambamo muna masomo 24 kwa miezi 6, vitatumiwa. Ni mwalimu ndiye atagawa masomo A4 kwa mwezi. Kila wiki kartasi itajazwa kwenye kanisa ao shule, ao itapelekwa kwa mtoto na kurudishwa yenye kujazwa, baada ya wiki moja. Mwisho wa kila mwezi, mwalimu atachukua masomo na ataipatia ma pointi; atairudisha kwa wanafunzi yenye kurekebishwa, kwa haraka iwezekanavyo.

Iliyo vema, vitabu vya muundo wa A5 vinapaswa kuchukuliwa na kupewa ma pointi mwisho wa kila mkutano, lakini mara nyingi tunaona kwamba haiwezekane. Katika kesi hii, ni vema kuigawa kwa wanafunzi wengine, na mwalimu ataleta ma pointi kwa masomo akisema kwa sauti wakati wanafunzi watakuwa wanarekebisha na kuweka alama katika masomo ya wenzao. Katika ukurasa wa mwisho wa kila kitabu, kuna fasi ambayo inaruhusu kuandika kiwango cha mafanikio cha kila mwezi, na pia maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Kwenye cheti hiki inaonekana nambari ya kiwango cha mafanikio kwa mwanafunzi muda wa miezi sita ya masomo.

## MASHAURI YA MUHIMU KWA WALIMU

Hapa, lengo siyo kwamba ni maagizo kwa walimu na kuwanyima uwezekano wote wa kulinganisha somo, kufuatana na mawazo na mipango yao wenyewe. Ni mapendekezo tu ambayo inaweza kusaidia katika utumizi wa mafundisho ya “wakati wa Biblia”.

- **Kujua historia vizuri –** Mwalimu anapaswa kufanya yote iwezekanayo ili ajue vizuri historia ya Biblia, vilevile mafundisho ya “wakati wa Biblia” ambayo inaambatana nayo. Iliyo vema ni kwamba amalize yeye mwenyewe kujifunza somo kabla ya kuwaambia watoto. Maelezo ya mwongozo inapaswa pia kusomwa na uangalifu kwa kusaidia katika kupangwa kwa kila somo.
- **Kuelewa mafundisho ya kushika –** Juu ya kila ukurasa, unaweza kusoma: “tunajifunza kwamba”, inafuatiwa na nukta mbili kubwa ambayo tunatumaini kwamba watoto wataelewa kisha kusikia maelezo ya mwalimu na kisha kujifunza mafundisho ya “wakati wa biblia”. Nukta kubwa ya kwanza inaelekea ufahamu na uelewa wa historia. Ya pili inatia watoto moyo kwa kushika kibinafsi mafundisho inayopatikana katika historia hiyo. Ma nukta kubwa hii ya kushika inafanya muhtasari wa ukweli muhimu ambao ulifundishwa katika somo. Mwalimu anaweza kuitumia kwa “kujipima kibinafsi” kutokana na mafundisho iliyopewa, pia uelewa wa watoto.
- **Kutanguliza –** Mafundisho yote inaanza kwa kuambatanishwa na mambo ambayo watoto wenyewe waliishi, inayofanana na jambo ambayo inaelezwa katika historia. Mawazo mengi yamependekezwa juu ya kutanguliza hadisi na kuwezesha watoto wajifunze kwa bidii tangu mwanzo wa huu wakati wa mafundisho ya Biblia.
- **Kufundisha –** Ma nukta kubwa za historia zimetajwa. Tunatumaini kwamba mwalimu hatakuwa anaisoma wakati anaieleza. Lakini, lazima ajue vizuri historia ili aweze kuisema kwa bidii na kuamsha akili. Atafanya kwamba wanafunzi waelewe mafundisho kubwa ya kushika na atawaongoza katika jinsi wanaweza kujibu na kuitumia. Tulijaribu, ilivyowezekana mara kwa mara kutoa maelezo fulani wakati historia inapoelezwa. Hiyo inaonekana kila mara katika maandishi ya *italiki*.
- **Kujifunza –** Kila historia inaambatana na shairi muhimu. Wakati mwingine kuna mbili, kama ya pili iliongezwa, inaweza kuwa mwepesi kukamata katika akili. Tunatumaini kwamba watoto watajifunza vizuri ma shairi muhimu na mara kwa mara watakuwa na nafasi kwa kuirudia juu ya kuikumbuka vema.
- **Kujaza somo –** Ikiwa masomo inafundishwa katika shule, mwalimu atajua kama watoto wanaweza kujaza masomo pekee ao kama wanahitaji kusaidiwa. Ikiwa ni lazima, inapaswa mwalimu awasomee maandiko ya somo watoto wengine ambao hawataweza kusoma pekee. Katika kesi moja kama katika nyingine, inaweza kuwa ya mafaa kuamsha akili ya wanafunzi katika ma nukta moja ambayo inapatana na maswali.

Kama mafundisho ya “wakati wa biblia” inatumiwa katika mazingira ingine isiyokuwa shule, ni ya muhimu kwamba mwalimu awe mwema na tayari kusaidia watoto ili mafundisho hii isionekane kuwa kitu cha magumu na cha kuchokesha, lakini kwa tofauti ionekane kuwa wakati wa kufurahisha. Ni ya muhimu pia kuwatia moyo watoto na kuwapongeza wakati wanapojifunza.

- **Kurudia –** Maswali na / ao michezo kidogo imepewa juu ya kurahisisha majifunzo na marudio ya historia.
- **Kuonyesha –** Katika ma kesi nyingine, tunajua kwamba inaweza kuwa magumu kuwa na vyombo vya kuonyesha picha. Lakini ikiwezekana, ni ya muhimu sana kuonyesha picha ao vitu ambavyo vitasaidia watoto kuelewa historia kwa njia ya mifano. Tunakushauri kutembelea tovu www.freebibleimage.org ambayo inaleta picha nyingi za ajabu za historia ya biblia. Kuandika tu jina ya yule aliye katika historia, katika kiingereza (kila mara), kwa mfano “Noah and the Ark”, msururu mzima wa ma picha inayomuelekea inaweza kupakuliwa kwa bure. Eikon Bible Art (www.eikonbibleart.com) inaleta pia vyombo vya kuonyesha picha lakini vifaa vyake ni vya kuuza. Ikiwezekana, mifano iliyo katika mafundisho ya “wakati wa biblia” inaweza kunenepeshwa na fotokopi, kisha kuwekwa rangi na kutumiwa kwa kuonyesha picha.

## Kufundisha mstari muhimu

Shairi inaweza kuandikwa katika karatasi kubwa ao katika kibao. Kisha, maneno mengi inaweza kuondoshwa polepole wakati watoto wanatamka shairi, mpaka wakati hakutabaki tena neno hata moja na wafikie kutamka shairi yote mzima, bila kusaidiwa.

Kwa kutanguliza mstari muhimu unaweza kutumia:

1. Mchezo wa kujaza visanduku: Mstari muhimu inaandikwa na herufi nyingi ambazo zinakosekana, hakuna neno inayo herufi zote. Watoto wanapendekeza herufi juu ya kujaza ma tundu, mpaka wakati mmoja wao anatambua shairi.
2. Kila mtoto eko na Biblia na wote wanafukuzia ili wavumbue shairi wa kwanza. Wa kwanza kuipata lazima aisome kwa sauti kubwa.

## Kusimamia muda

- Maelezo yote yameundwa namna moja, ikilinda taratibu moja ya sehemu tofauti. Lakini ikiwa ya lazima, mwalimu anaweza kubadilisha muundo.
    1. Kueleza na kufundisha historia: Karibu dakika 15,
    2. Kujifunza Mstari muhimu: karibu dakika 5 mpaka 10
    3. Kujaza karatasi: dakika 20
    4. Michezo na ma kazi nyingine: dakika 5 mpaka 10.

Kumbuka haya:

“Uniambie na mimi nitasahau,
Unionyeshe na nitakumbuka,
Unishirikishe na nitaelewa”

## Kitabu cha Wakati wa Biblia

| | Kiwango 1 (miaka 5-7)<br>Kiwango 2 (miaka 8-10) | Kiwango 3 (miaka 11-13) | Kiwango 4 (miaka 14+) |
|---|---|---|---|
| **MSURURU A** | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Abrahamu<br>6. Abrahamu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa kwanza<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji na kuanguka<br>2. Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya kikristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas |
| **MSURURU B** | 1. Utoto wa Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Mafumbo<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Yesu anakutana na watu<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Waandishi wa Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Bwana Yesu<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Maisha ya Yosefu<br>8. Njia ya kwenda<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Sheria<br>12. Muujiza wa Krismas |
| **MSURURU C** | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Historia ya pasaka<br>5. Ruta na Esiteri<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu waliotumiwa na Mungu<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Yesu ine<br>3. Nguvu ya Bwana<br>4. Bwana Yesu<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu wa Agano la Kale<br>12. Kuzaliwa kwa Kristo |

## A7 SOMO 1
**Petro anatangaza Neno la Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Ilikuwa ni lazima kwa wanafunzi kupokea Roho Mtakatifu.<br>• Roho Mtakatifu anaishi ndani ya wote ambao wanatia tumaini lao ndani ya Bwana Yesu kama Mwokozi wao.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 2:36***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 2:1-14, 36-39*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uliza ma swali kwa ajili ya kuanzisha mafundisho kuhusu Roho Mtakatifu. Unaweza kuona upepo? Hapana. Unajua namna gani kwamba iko? Unaweza kuona kile inafanya. Ikiwa inawezekana kuangalia inje, tafuteni alama za upepo zinazoonekana.<br>• Kumbusha historia ya Pasaka. Yesu alikufa na kufufuka. Kabla ya kuondoka dunia ili arudi mbinguni, aliahidi kutuma kwa wanafunzi wake msaidizi wa pekee sana, lakini asiyeonekana.<br>• Ilikuwa ni "nguvu" inayoitwa Roho Mtakatifu ambaye atakuja kukaa ndani ya kila moja wao. Kama vile upepo, hataonekana, lakini wanafunzi watatambua tofauti ambayo anafanya katika Maisha yao. |
| **KUFUNDISHA** | • Muda kidogo baada ya kurudi kwa Yesu mbinguni, wanafunzi wanajikuta wamekusanyika ndani ya nyumba kule Yerusalema. ***(Matendo 2:1-4)*** Gafula, uvumi kama upepo unaovuma ukajaza nyumba yote. Na zilionekana kwao ndimi kama za moto zikawakalia kila mmoja wao. Roho Mtakatifu amekuja! *Kulingana na wewe, wanafunzi walijisikia namna gani wakati zawadi hii ya ajabu ilipokuja? (Furaha, mshangao, walifurahi kwa kuona utimilifu wa ahadi ya Yesu).*<br>• Kisha, wanatambua kwamba wanasema lugha zingine! *Eleza kwamba kwa kawaida, tunasema tu ma lugha ambazo tulijifunza kwa wazazi yetu tangu utoto wetu, ao zile tulifundishwa hapo shuleni. Wanafunzi wa Yesu hawakujifunze lugha zingine.* Alama hizi zote zilionyesha kuja kwa Roho. *Ungewaza je ikiwa wewe ulipita pahali pale wakati ule?*<br>• Watu ambao walikuwa pembeni walisikia kelele. Walishangaa pia walikuwa na maulizo mengi! ***(Matendo 2:5-13)***<br>• Petro alishika muda ule ili awafasilie mambo ambayo ilifanyika na kuwaambia Habari ya Bwana Yesu. ***(Matendo 2:36-39)*** *Eleza magumu iwezekanayo ya Petro kwa kusema mbele ya kundi kubwa (inaweza kuogopesha, inapaswa kupata maneno muzuri, watu watajibu namna gani?)*. Lakini Petro aliweza kuifanya kwa sababu Roho Mtakatifu alimsaidia.<br>• *Wale ambao walimsikia Petro walihitaji kuokolewa katika zambi zao, kama vile sisi.*<br>• *Eleza kwamba Roho Mtakatifu amepewa kwa kila mtu anayemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi. Roho Mtakatifu atatusaidia kuwaambia wengine kuhusu Yesu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 2:36***. Hii iko katika ile Petro alisema wakati alihubiri. Aliwaambia watu kwamba ni wao walimuua Yesu, lakini Mungu alimfufua. Ile inaonyesha kwamba Yesu hakuwa mwanadamu tu, lakini alikuwa Bwana na Kristo. |
| **KURUDIA** | • Mitume walikuwa wapi wakati Roho Mtakatifu alipokuja?<br>• Kelele ilifanana na nini wakati alikuja?<br>• Mitume waliona nini?<br>• Walifanya nini wakati walijazwa na Roho Mtakatifu?<br>• Ni nani alikisia mambo ambayo ilifanyika?<br>• Ni mtume gani ambaye alisimama kwa ajili ya kufasilia mambo ambayo ilifanyika?<br>• Petro alisema habari ya nani?<br>• Kulingana na Petro, watu walipaswa kufanya nini juu ya zambi zao?<br>• Ni zawadi gani ambayo waliweza kupata ikiwa wanafanya vile?<br>• Roho Mtakatifu anaishi ndani ya watu gani leo? |

## A7 SOMO 2
**Petro anaponya kiwete**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Nguvu ya Yesu ilitenda kupitia Petro na Yoane kwa kumponya huyu kiwete.<br>• Petro na Yoane walitaka kumsaidia mtu huyu. Tunapaswa kutafuta kusaidia wengine.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 3:6 (kiwango 1); Matendo 3:16 (kiwango 2)***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 3:1-12*** |
| **KUTANGULIZA** | • Eleza kwa huruma mtu aliye kiwete, ambaye hakuweza kutembea. Alipaswa kuomba ili anunue chakula.<br>• Ikiwezekana, onyesha bakora, lakini fasilia kwamba mtu huyu alipaswa kuchukuliwa na marafiki zake.<br>• Onyesha picha ya mtu mwenye huzuni kama mfano wa mtu huyu. |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja, Petro na Yoane walikuwa wakipanda pamoja Kwenda hekaluni, mtu moja kiwete aliwaomba sadaka. ***(Matendo 3:1-5)*** *Tia mkazo katika jambo la kwamba walichukua muda wa kusimama karibu naye.*<br>• Tumia maneno moja na Petro. “Sina feza wala zahabu, lakini nilicho nacho ninakupa. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama utembee! ***(Matendo 3:6-7)*** *Fasilia kwamba feza na zahabu vingemsaidia mtu huyu kwa muda kidogo tu lakini angeendelea kushindwa kutembea.* Petro alimpa kitu ambacho kiliweza kubadilisha kabisa maisha yake.<br>• Petro anamshika mkono na kumunyanyua. Mara moja miguu yake na vifundo vya miguu yake vinapata nguvu. Anaweza kutembea na kurukaruka kwa mara ya kwanza maishani mwake! Moyo wake umejaa sifa kwa Mungu na ameingia hekaluni pamoja na Petro na Yoane. ***(Matendo 3:8)*** *Onyesha picha moja ya uso wa furaha, iliyo tofauti na ile ya kwanza. Ungewaza nini ikiwa ulizoea kumuona kiwete huyu, akiomba sadaka siku zote?*<br>• Wote wameshangaishwa na mambo ambayo inafanyika. ***(Matendo 3:9-12)***<br>• *Zungumzieni pamoja jinsi tunaweza kuiga mfano wa Petro. Mubebe mifano ya msaada tunaoweza kuwapa wengine, ambao tunaweza kusaidia wengine. Sema pia kwamba kitu cha muhimu sana ambacho tunaweza kugawana, ni Habari Njema ya Bwana Yesu.*<br>• *Kama vile mtu huyu, tuko pia na magumu maishani mwetu. Nguvu ya Yesu inaweza kuondoa zambi yetu. Kama vile mtu huyu aliwekwa huru katika ulemavu wake wa kimwili.*<br>• *Fikirieni vitu kwa ajili ya hivyo tunaweza kushukuru Mungu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Matendo 3:6* (kiwango 1), ao *Matendo 3:16* (kiwango 2)**. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. *Ikiwa inaonekana kuwa ya mafaa kwako, watoto wanaweza kutamka mstari muhimu wakitembea, wakirukaruka.* |
| **KURUDIA** | • Ilikuwa saa ngapi?<br>• Petro na Yoane walikuwa wanaenda wapi?<br>• Mtu huyu hakuweza kutembea tangu wakati gani?<br>• Mtu huyu alikuwa amewekwa pahali gani kila siku?<br>• Aliomba nini kwa Petro na Yoane?<br>• Petro alimponywa mtu huyu kwa jina la nani?<br>• Petro alifanya nini zaidi ya kusema na mtu huyu?<br>• Taja vitu tatu ambavyo mtu huyu aliweza kufanya kutokana na muujiza huu?<br>• Alienda wapi baada ya kuponywa?<br>• Nguvu ya Yesu inaweza kufanya nini maishani mwetu? |

<u>**A7 SOMO 3**</u>

**Petro katika kifungo**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Wakristo wa kwanza walijikuta katika upinzani wa wakubwa wa dini ambao walimsulubisha Bwana Yesu.<br>• Wale ambao wanampenda kweli Yesu watamtii, ingawa magumu yao.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 13:6***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 4:1-22*** |
| **KUTANGULIZA** | • Kwa sababu somo hii inaendeleza historia ya somo iliyotangulia, ni vizuri kubeba muda wa kuirudia tena.<br>• Tumia ma picha za nyuso ya furaha na ya huzuni kwa ajili ya kukumbusha historia.<br>• Mtu huyu aliponywa namna gani? Tia mkazo katika nguvu ya Yesu ambaye aliwezesha muujiza huu. |
| **KUFUNDISHA** | • Kisha, Petro na Yoane walihubiri Bwana Yesu aliyefufuka na watu wengi waliamini. ***(Matendo 4:1-2, 4)***. Lakini wakubwa wa dini walifazaika sana kwa sababu Petro na Yoane walihubiri ufufuko wa Yesu. Mara moja wakakamata Petro na Yoane na wakawaweka katika kifungo. ***(Matendo 4:3)*** *Eleza jinsi jambo hili iliweza kufanyika kwao, na walijisikia namna gani.*<br>• Asubui, wakawaondosha katika kifungo ili wawalete mbele ya wakubwa wa dini. ***(Matendo 5:5-7)*** *Eleza kwamba kundi hii ilipaswa kuamua kama mitume walikuwa pasipo kosa ao wenye kosa.*<br>• Mara tena, Roho Mtakatifu alimsaidia Petro kueleza namna gani mutu yule aliponywa. ***(Matendo 4:8-12)*** Wakubwa wa dini wakashindwa namna ya kujibu! Wakalazimishwa kutambua kwamba muujiza kubwa ulifanyika. Baada ya kuzungumza pamoja, wakaamua kukataza Petro na Yoane kusema ao kuhubiri kwa jina la Yesu. ***(Matendo 4:13-19)*** *Petro na Yoane waliwaza nini kwa hiyo? Walitii?*<br>• Petro na Yoane walijua kwamba haitawezekana kwao wasiseme kuhusu Bwana Yesu! ***(Matendo 4:20)*** *Mapendo yao kwake ilikuwa kwamba waliamua kabisa kumtii. Walijua kwamba wataweza kutegemea uwepo wa Bwana, ingawa mambo itakayotukia. Roho Mtakatifu atawasaidia.*<br>• *Yesu alituomba pia tumpende na kumtii, hata kama iko magumu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Waebrania 13:6***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. Fanyeni “mchezo wa kutamka” sentensi ya kwanza pia shairi yake, kabla ya kuongeza baki la mstari. Tenganisha watoto katika ma kundi tatu na kila kundi inaweza kusema sehemu moja ya mstari, na wote pamoja watataja shairi yake. *Munawaza kwamba maneno hii iliweza kusaidia Petro na Yoane? Uwaelezee watoto kwamba inaweza kutusaidia, sisi pia!* |
| **KURUDIA** | Tayarisha mchezo wa “kweli-uwongo”. Andika ma sentensi iliyo hapa chini katika kibao na weka katika kila moja ma pointi (kati ya 5 na 100). Kisha uziweke katika mfuko. Uwatenganishe watoto katika ma kundi mbili ambayo itachanga ma pointi yao.<br>• Polisi ilimkasirikia Petro na Yoane.<br>• Walikaa katika kifungo usiku moja.<br>• Asubui, Petro na Yoane walipelekwa mbele ya wakubwa wa dini<br>• Petro aliambia watu hawa kwamba nguvu ya Yesu ilimponya kiwete.<br>• Roho Mtakatifu alisaidia Petro na Yoane kusema mbele ya baraza hii?<br>• Petro na Yoane walikimbia.<br>• Wakubwa wa dini waliamua kwamba Petro na Yoane hawakuwe tena na ruhusa ya kusema kuhusu Yesu.<br>• Petro na Yoane walilaka kwamba watatii wakubwa. |

## A7 SOMO 4
**Petro amewekwa huru**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu analeta nguvu yake na msaada kwa wakristo ili waweze kumfanyia kazi<br>• Maombi ni ya muhimu wakati wote.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ama Matendo 4:31, ao Matayo 6:33***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 4:23-31*** |
| **KUTANGULIZA** | • Zungumza na Watoto kuhusu vitu ambavyo wanatamani kugawana na familia zao ao marafiki zao. Kwa jumla, wanapendelea kueleza vitu vigeni ambavyo walifanya, kama vile matembezi ao mchezo wa kupiga mbio. Wakati mwingine weko na wasiwasi, na kuigawana na wenzao inaweza kuwafariji. |
| **KUFUNDISHA** | • Petro na Yoane walikuwa na Habari ya kuambia marafiki zao. ***(Matendo 4:23)*** Kumbusha kwamba Habari njema, ni kwamba walitoka katika kifungo, lakini habari mbaya ni kwamba waliwakataza kusema kuhusu Yesu!<br>• Marafiki za Petro na Yoane walifanya uamuzi muzuri: walienda kuomba. ***(Matendo 4:24-30)*** Walijua kwamba Mungu anatawala kila kitu. Yeye ni mwenye nguvu sana zaidi ya wale ambao walitafuta kukamata mitume. Walipoomba, walikumbuka matendo ya Mungu ya ajabu wakati wa zamani ambayo inaonyesha nguvu yake. Waliomba Mungu awape ujasiri na wafanye miujiza ingine kwa jina na nguvu ya Yesu. ***(Matendo 4:29-30)***<br>• Mwisho tu wa maombi yao, Mungu alijibu! ***(Matendo 4:31)*** *Eleza kwamba pahali pale palitetemeka kwa sababu Mungu aliwaonyesha tena nguvu ya Roho Mtakatifu ambaye atakuwa nao kwa kuwasaidia kuhubiri Bwana Yesu.*<br>• *Sema kwamba sisi pia, tunaweza kuomba wakati tuna mambo ambayo ni magumu kwa kuifanya.*<br>• *Mungu anasikia maombi yetu na anajibu. Atatusaidia kumpa Bwana Yesu fasi ya kwanza, kama vile aliifanya kwa watu walio ndani ya historia ya leo.*<br>• *Na Watoto wa kiwango cha 2, munaweza kuzungumza kuhusu wakristo ambao wanaishi katika ma inchi mwenye imekatazwa kugawana Habari njema ya Yesu. Tunaweza kuomba kwamba wawe na ujasiri wa kumpa Yesu pahali pa kwanza.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Matendo 4:31*, ao *Matayo 6:33***. Kuhusu hii ya pili, eleza kwamba katika ufalme wa Mungu muna vitu vyote ambavyo ni vya muhimu kwa Mungu, hakika Yesu Kristo pia. |
| **KURUDIA** | Hapa chini, kuna daftari ya ma swali ya kuuliza kuhusu masomo 4 ya A7.<br>• Kwa sababu ya nini wanafunzi wa Yesu walihitaji Roho Mtakatifu?<br>• Wanafunzi waliona nini wakati Roho aliposhuka<br>• Jaza mstari muhimu wa Somo 1: "Mungu amefanya huyu Yesu ambaye mulimsulubisha kuwa_______________na ___________." ***(Matendo 2:36)***<br>• Kwa sababu ya nini yule mtu alikuwa hekaluni alikuwa analomba?<br>• Hakuweza kutembea tangu wakati gani?<br>• Jaza mstari muhimu wa Somo 2: "Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ____________ _____________" ***(Matendo 3:6)***<br>• Muujiza huu ulionyesha nini kwa watu kuhusu Bwana Yesu?<br>• Kwa sababu ya nini waliweka Petro na Yoane katika kifungo?<br>• Wakubwa wa dini waliwakataza nini?<br>• Ni nini ilifanyika wakati Mungu alijibu maombi ya marafiki za Petro na Yoane? |

**A8 SOMO 1**
**Petro anamsaidia Tabita (Dorika)**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Nguvu ya Bwana ilitenda kupitia Petro wakati alimponya Tabita.<br>• Tunapaswa kumjibu Bwana Yesu kwa imani<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 9:42***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:32-43*** |
| **KUTANGULIZA** | • Muzungumzie pamoja jinsi tunaweza kusaidia walio katika hitaji kwa kuwagawia vitu tunavyo. Unaweza kuionyesha kupitia mifano inayoonekana.<br>• Eleza kwamba Tabita (Dorika) ni mwanamke mwenye ukarimu sana ambaye alimpenda Bwana Yesu. Ndiyo sababu alikuwa akipitiza muda wake katika kusaidia wengine. Alikuwa mwenye ujuzi wa kushona na alikuwa anashona nguo kwa ajili ya masikini. |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja, Tabita akagonjwa na akakufa. ***(Matendo 9:37)*** *Marafiki zake walijisikia namna gani?*<br>• Kisha watu wawili walienda kumtafuta Petro ambaye alikuwa katika mji jirani ulioitwa Yopa. ***(Matendo 9:38)***<br>• Mara moja Petro akaenda kwa Tabita. ***(Matendo 9:39-41)*** *Eleza historia ukifuata hatua zote. Kabla, Petro akaomba, kisha akasema na Tabita, akamshika mkono na akamsaidia kusimama. Tabita akakuwa hai tena. Onyesha tofauti iliyo kati ya kuzidi kwa furaha na huzuni ambavyo Petro alikuta wakati alipofika. Sema kwamba huu ni muujiza ambao Petro alifanya kwa sababu tu ya nguvu ya Bwana Yesu iliyo ndani yake.*<br>• Watu wengi wakamwamini Bwana Yesu. ***(Matendo 9:42)***<br>• *Tunapaswa kumwamini Bwana Yesu, kama vile wale ambao walimuona Tabita amefufuliwa.*<br>• *Eleza kwa maneno rahisi maana yake: Tunapaswa kuamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, kwamba yeye ni hai, na yeye ana uwezo wa kuondosha zambi zetu. Kumwamini Yesu inamaanisha kutia tumaini letu ndani yake.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 9:42***. *Huu mstari muhimu ni rahisi kujifunza hata kwa watoto wadogo. Lakini chunguza kama wanaelewa vizuri maana yake. Ni nani aliamini? Ni nini ilifanya kwamba waliamini? Kwa nini ni ya muhimu kumwamini Bwana? Mtu anaweza kumwamini Bwana namna gani?* |
| **KURUDIA** | • Tabita aliishi wapi?<br>• Alikuwa anasaidia wengine namna gani?<br>• Kwa sababu ya nini alikuwa anawasaidia?<br>• Watu walijisikia namna gani wakati Tabita alipokufa?<br>• Ni nani alienda kumtafuta Petro?<br>• Petro alifanya nini wakati alipiga magoti pembeni ya Tabita?<br>• Petro alisema nini?<br>• Alifanya nini baada ya kusema naye?<br>• Watu wengi walifanya nini baada ya muujiza?<br>• Shairi ya mstari muhimu ni nini? |

## A8 SOMO 2
**Petro anapata ono**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Petro alikuwa mtiifu. Alifanya ile Mungu alimuomba.<br>• Mungu anapenda dunia yote na anataka kwamba wote wasikie Habari njema ya Bwana Yesu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 3:16***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 10:9-23*** |
| **KUTANGULIZA** | • Sema kuhusu ma tofauti fulani kati ya watu kulingana na inchi zao kwenye wanatoka.<br>Tumia picha ao taswira ikiwa inahitajiwa.<br>• Sema kuhusu ma tofauti kama rangi ya Ngozi, nyole ao lugha.<br>• Mungu aliumba watu wote. Anataka kwamba kila mtu asikie habari yake na Mwana wake, Bwana Yesu. |
| **KUFUNDISHA** | • Wakati Petro alikuwa anaomba kule Yopa (uipatanishe na A8 Somo 1), Mungu alimuonyesha kwamba alipenda watu wote. ***(Matendo 10:9-16)*** *Hakuna lazima ya kuingia katika maelezo mengi ya ono hii. Kwa watoto wa kiwango 2, unaweza kueleza kwamba ukweli huu ulikuwa magumu kwa Petro kuuitika kwa sababu alikuwa muyuda na ule wakati, alikuwa anawaza kwamba wayuda pekee yao ndio walikuwa wenye bei kwa Mungu. Alipaswa kujifunza kwamba watu wote ni wenye maana mbele ya Mungu.*<br>• Watu tatu wanafika na kumwita Petro aende nao pamoja kwa Kornelio. ***(Matendo 10:17-22)*** *Eleza kwamba Kornelio alikuwa akida wa kiroma mwenye kuheshimiwa ambaye alikuwa mwenye haki na kuogopa Mungu.* Kornelio hakuwe na rangi moja na Ptero na kwa kawaida, Petro hakufai kutembelea mtu kama Kornelio. *Eleza kwamba hata hivi, Petro alijua kwamba alipaswa Kwenda kule, ya kwanza kwa sababu Mungu alimuambia kuifanya, kisha kwa sababu alikuwa anajiacha kuongozwa na Roho Mtakatifu.*<br>• Petro alienda hata katika nyumba ya Kornelio kule Kaisaria, kwenye urefu karibu 70km. ***(Matendo 10:23)*** *Saidia watoto kuona urefu huu kwa kuulinganisha na safari ambayo wanajua. Ilifanya siku mzima. Sema kwamba kwa kufanya safari hii, Petro alimtii Mungu.*<br>• *Tia mkazo katika ukweli wa kwamba Mungu anataka kwamba wote, bila ubaguzi, wajue kwamba anawapenda. Alituma Mwana wake kufa msalabani ili watu wote wasamehewe.*<br>• *Uwaeleweshe Watoto kwamba, kama wamekwisha kutia tumaini lao ndani ya Bwana Yesu, sasa wanaweza kusaidia watu wengine wamjue.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Yoane 3:16***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Petro alikuwa anakaa kwa nani?<br>• Petro alikuwa anafanya nini na saa sita?<br>• Mungu alitaka kumpa Petro ujumbe gani wakati sauti ilisema naye?<br>• Ni watu ngapi walikuja kumuona Petro?<br>• Petro alipaswa kutembelea nani?<br>• Kazi ya Kornelio ilikuwa kazi gani?<br>• Kwa sababu ya nini Petro alienda kwa Kornelio?<br>• Mungu alionyesha namna gani mapendo yake kwa ajili ya dunia yote?<br><br>**Maonyesho:** Munaweza kurudia sehemu ya historia pale watu wanafika kwa Petro. Ile inaweza kuendelea katika somo inayofuata. Watu wazima wanaweza kufanya mchezo kama Petro na wale watu tatu. |

**A8 SOMO 3**
**Petro na Kornelio**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Kornelio alikuwa mmoja kati ya wasio wayuda (wapagano) walioamini Yesu.<br>• Mungu ni tayari kusamehe zambi za mtu yeyote anayemwamini.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 10:43***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 10:23-48*** |
| **KUTANGULIZA** | • Kwa sababu somo hii ni kuendelea kwa historia ya Somo 2, unaweza kurudia ma swali kidogo ya Somo 2 kama ukumbusho.<br>• Kisha, unaweza kuwapa watoto mfano wa tukio moja ya muhimu katika jamii lenu ambayo inakusanya watu wengi ambao wanakuja kusikia hotuba, mafundisho fulani… |
| **KUFUNDISHA** | • Petro alifika nyumbani mwa Kornelio. ***(Matendo 10:24-33)*** Uwasaidie watoto kufikiria tukio hii (nyumba imejaa, jamaa na marafiki za Kornelio, wote wanataka kumuona Petro). Kama vile Kornelio anataka kumuheshimu Petro, anamwangukia kwenye miguu na anamwabudu! Lakini mara moja Petro anamsimamisha akimwambia kwamba haifai kuabudu mtu tu. Kisha Kornelio anajibu kwamba Mungu alimwambia atume watu kumtafuta Petro. *Unaweza kuwaambia Watoto kwamba Mungu alikuwa anatayarisha mmoja na mwingine kwa sababu ya kukutana huku!*<br>• Ujumbe wa Petro. ***(Matendo 10:34-43)*** *Eleza kwamba Petro alisema kwamba Mungu anataka watu wote wa ma taifa yote wamwamini.*<br>• Sema kuhusu maelezo ambayo Petro anawapa kuhusu Bwana Yesu: Alitenda mema, aliponya wagonjwa, aliuawa lakini Mungu alimfufua. Bwana Yesu atakuwa mwamzi siku moja, lakini kitu cha muhimu zaidi ya vyote, ni kwamba anasamehe wote ambao wanamwamini tangu sasa.<br>• Jibu ya wale ambao walisikia. ***(Matendo 10:44-48)*** Roho Mtakatifu alisaidia watu hawa kuelewa maana ya ile Petro alitoka kuwaambia. Walimwamini Bwana Yesu na zambi zao zilisamehewa.<br>• *Eleza kwamba wakati tunasikia Habari njema ya Bwana Yesu, tunapaswa kuwa na jibu namna moja na watu hawa. Kwa kutia tumaini letu ndani yake, sisi pia, tunaweza kusamehewa.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 10: 43***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | Kuliko kuuliza ma swali, itapendeza kubandika ma picha za nyuso kando ya mstari muhimu ulioandikwa kwa herufi kubwa. Kila mtoto anaweza kuchora uso wake. Ile itakazisha ukweli ambao Petro alijifunza kuhusu mapendo ya Mungu kwa wote. Tia mkazo katika jambo la kwamba Mungu anapenda kila mtu kibinafsi. Ao, ikiwa uko na ma Gazeti, Watoto wanaweza kukata nyuso ili waibandike baadaye pembeni ya mstari huu.<br><br>**Maonyesho:** Historia hii inaweza kufanyika kupitia mchezo, kama ilivyopendekezwa katika Somo 2. |

<u>**A8 SOMO 4**</u>

**Petro (mara tena) katika kifungo**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Marafiki za Petro walimuombea.<br>• Mungu anaweza kuchagua kufanya vitu vya ajabu kama jibu ya maombi yetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yakobo 5:16***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 12:1-19*** |
| **KUTANGULIZA** | • Musemee simu na mafaa yake, iwe kwa ajili ya kuzungumza na marafiki zetu ao kuomba msaada. Ikiwezekana, tumia simu ya mkono kama mfano.<br>• Rudieni katika ufafanuzi wa maombi: kusema na Mungu. Asitupe jibu kwa sauti, lakini kila mara anasikia. Ana uwezo wa kujibu maombi yetu.<br>• Katika historia ya leo, kundi la marafiki waliombea kitu moja cha muhimu. |
| **KUFUNDISHA** | • Petro katika kifungo. ***(Matendo 12:1-4)*** Mfalme Herode alikuwa mwenye kuchukia wanafunzi wa Yesu. Alimwua Yakobo kwa upanga. Baada ya muda kidogo, Petro alikamatwa na kutupwa katika kifungo. Uwakumbushe mara ya kwanza ambayo ilimfikia (Matendo 4, A7, Somo 3).<br>• Maombi ya marafiki za Petro. ***(Matendo 12:1-4)*** *Muzungumze pamoja kuhusu sababu ya nini ilikuwa kitu kizuri zaidi cha kufanya*.<br>• Amefunguliwa kutoka kifungo. ***(Matendo 12:6-10)*** Ile ilifanyika usiku wa siku ile Petro alipaswa kupelekwa mbele ya waamzi *(eleza namna gani maamuzi ya hii baraza ilikuwa ya muhimu).* Petro alikuwa mwenye kufungwa mnyororo kati ya waaskari wawili, lakini alikuwa amelala. Leta maelezo mengi kupitia picha kufunguliwa kwa Petro na malaika. Uwaonyeshe mshangao wa Petro mbele ya mambo ambayo inamfikia. Anawaza kwamba anapata maono!<br>• Petro katika nyumba ya marafiki zake. Alipojikuta njiani, anatambua kwamba Mungu amemuweka huru. *Anapaswa kujisikia namna gani?* Akaenda kwa haraka kwenye nyumba ya marafiki zake. ***(Matendo 12:11-17)*** Fasilia jinsi Roda alikaribia kwenye mlango, mara ya kwanza asikuufungula, pia tendo la marafiki wengine ambao walikuwa nyumbani. Walikuwa na sababu ya kushangaa pia?<br>• *Muzungumzie pamoja mambo tofauti ambayo tunaweza kuleta kwa Mungu katika maombi. Kila mara Mungu anasikia maombi yetu na anaijibu mu namna muzuri sana.*<br>• *Hatupaswi kusahau kumushukuru Mungu na kumusifu wakati anapojibu maombi yetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Yakobo 5:16***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. Mstari huu unaonyesha namna gani maombi yetu ni ya bei. Mungu anaitumia kwa ajili ya kutimiza kazi yake. |
| **KURUDIA** | • Ni nani alimuweka Petro katika kifungo?<br>• Ni nani ambaye kabla aliuawa na Herode?<br>• Petro alikuwa anafanya nini wakati Mungu alituma Malaika?<br>• Kwa nini marafiki za Petro walikutana Pamoja?<br>• Malaika alimwambia Petro afanye nini?<br>• Petro alipita namna gani mlango wa kifungo?<br>• Malaika alibaki pamoja na Petro saa ngapi baada ya kutoka katika kifungo?<br>• Kisha Petro aliendа katika nyumba gani?<br>• Ni nani alimupata Petro mbele ya mlango?<br>• Kwa nini Roda hakufungue mlango hapo mwanzo?<br><br>**Maonyesho:** Sehemu ya historia wakati Petro aliondoka katika kifungo inaweza kuonyeshwa na watu wawili katika mchezo. Mtoto moja anacheza kama Petro, na mwingine anacheza kama malaika. Mtu mzima anaweza kueleza historia, akieleza matendo ambayo watoto watafanya. |

## A9 SOMO1
## Yakobo anadanganya ndugu yake

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Kuwa mwenye ubinafsi inamaanisha kujijali wewe mwenyewe kwanza, hata kama inawaumiza wengine.<br>• Inaweza kutufikia kuwa wenye ubinafsi kama Yakobo, na ni zambi mbele ya Mungu<br><br>**Mstari muhimu:** ***Hama Mwanzo 25:28, ao Wafilipi 2:3***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 25:19-34*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uliza watoto kama wanajua mapacha. Weko tofauti ao wanafanana kuhusu tabia zao na uumbo wao kimwili? Mara zingine kuna mizozo kati ya ndugu na dada?<br>• Kuwa mwenye ubinafsi: maana yake nini? Ambia watoto wafikirie mfano wa kipekee wakati mtu ambaye wanajua alitenda mu namna ya ubinafsi, na ilifanya kwamba wateswe.<br>• Somo hii inaelekea ndugu wawili ambao hawakuwe wanaelewana muzuri. Moja wao alijipendelea mwenyewe, na alidanganya ndugu yake. |
| **KUFUNDISHA** | • Isaka na Rebeka walikuwa wanaongojea mapacha. Kabla ya kuzaliwa kwao, Mungu alimwambia Rebeka kwamba mukubwa atatumikia mdogo. ***(Mwanzo 2:19-23)***<br>• Tangu kuzaliwa kwa mapacha, ilionekana kwamba watakuwa tofauti kabisa moja na mwingine. Mzaliwa wa kwanza, Esau, mwili wake ulikuwa mwenye manyoya, lakini ndugu yake alikuwa na ngozi mrembo. ***(Mwanzo 25:24-26)*** Walikuwa pia na Mawazo tofauti. Esau alikuwa mwindaji mwenye ujuzi sana, lakini Yakobo alipenda kukaa chini ya hema. Kila mzazi alikuwa na mwana wake mpendwa. Isaka alipenda Esau, na Rebeka alipenda Yakobo. ***(Mwanzo 25:27-28)***<br>• Siku moja, Yakobo akapiga mboga. Esau alienda shambani. Saidia watoto kufikiria tukio hii: Esau amechoka na njaa, arufu ya mboga mzuri! Esau alitaka kula mara moja! Lakini Yakobo alikuwa mjanja sana. Kwa haraka akasema kwamba atampa Esau mboga kwa lazimisho ya kwamba amuuzishe haki yake ya mzaliwa wa kwanza. *Eleza maana ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Kulingana na kiasili, ni mzaliwa wa kwanza ndiye aliwekewa kupata haki hii. Ilimaanisha kwamba atakuwa kiongozi wa familia wakati wa kufariki kwa baba. Atapata pia sehemu ya mali ya baba yake mara mbili.*<br>• Esau hakubebe muda wa kuwaza, kwa sababu alikuwa na njaa kabisa! Aliangukia katika mtego uliopangwa na ndugu yake na aliuzisha haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa sababu ya bakuli ya mboga. ***(Mwanzo 25:29-34)*** *Muzungumzie pamoja kuhusu tabia ya hawa wana wawili. Yakobo alikuwa na sheria ya kumudanganya ndugu yake hivi? Esau alifanya muzuri kwa kuuzisha haki yake ya mzaliwa wa kwanza juu ya bakuli ya mboga tu?*<br>• *Unawaza kwamba mwenendo wa Yakobo na Esau ulimpendeza Mungu?*<br>• *Wakati mwingine, sawa Esau na Yakobo, tunawaza tu vitu ambavyo tunataka. Wakati sisi ni wenye ubinafsi, tunatenda zambi mbele ya Mungu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Mwanzo 25:28***, **ao *Wafilipi 2:3***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Vijana hawa wawili katika historia waliitwa kwa jina gani?<br>• Mzaliwa wa kwanza alikuwa nani?<br>• Taja ma eneo mule vijana hawa walikuwa tofauti moja na mwingine.<br>• Fasilia haki ya mzaliwa wa kwanza?<br>• Unawaza, kwa nini Yakobo alitaka yeye mwenyewe haki ya mzaliwa wa kwanza?<br>• Yakobo alidanganya ndugu yake namna gani?<br>• Tunaweza kujifunza ma somo gani katika historia hii? |

## A9 SOMO 2
**Yakobo anadanganya baba yake**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Rebeka na Yakobo walitaka kumudanganya Isaka.<br>• Kudanganya na kusema uwongo ni mubaya mbele ya Mungu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ama Mwanzo 27:20, ao Zaburi 32:2***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 27:1-29*** |
| **KUTANGULIZA** | • “Kusema uwongo” maana yake nini?<br>• Katika historia hii, Yakobo anasema uwongo kwa baba yake. Jambo hii ilimuumiza sana baba yake na ndugu yake.<br>• Ambia watoto wawaze kuhusu historia zingine ambamo uwongo wa mtu fulani uliumiza mtu mwingine. |
| **KUFUNDISHA** | • Isaka alikuwa mzee na kipofu. Alitaka kubariki mwana wake mzaliwa wa kwanza, Esau, kabla ya kufa. Sasa anamuomba Esau amutayarishie chakula cha kipekee. ***(Mwanzo 27:1-4)*** *Fasilia kwamba nyakati za Biblia, baba alikuwa anabariki mwana wake mzaliwa wa kwanza kabla ya kufa.*<br>• Rebeka amesikia kwamba Isaka ana nia ya kumbariki Esau. Yeye na Yakobo wakapanga mpango pamoja. Shabaa yao ni kumudanganya Isaka ili ambariki Yakobo pahali pa ndugu yake. Hivi, Rebeka akatayarisha chakula cha kipekee na akafunika mikono ya Yakobo kwa Ngozi ya mwana-mbuzi ili awe na manyoya sawa Esau. ***(Mwanzo 27:5-17)*** *Uwakumbushe watoto kwamba kila mzazi alikuwa na mwana wake mpendwa. Kwa Rebeka, ilikuwa Yakobo, na kwa Isaka, ilikuwa Esau. Kila mmoja alitaka kwamba mwana wake mpendwa apate baraka. Leta mfano wa upendeleo katika mazingira ya nyumba ao shule ambao watoto wataweza kutambua kwamba sio haki!*<br>• Yakobo anamuletea Isaka chakula cha kipekee. Anasema uwongo kwa baba yake, akijifanya kuwa Esau. Isaka ameshangaa kwa sababu Esau ametayarisha chakula hii muzuri kwa muda kidogo tu. ***(Mwanzo 27:18-20)*** *Unawaza Rebeka na Yakobo wanamupendeza Mungu? Kwa nini?*<br>• Isaka angali na mashaka. Ni Esau kweli? Anataka kusadiki, ndio sababu akaomba kugusa mikono ya Yakobo. Ndio, kwa kumugusa, ni Esau kweli, lakini sauti ni ya Yakobo. Isaka asielewe. Yakobo anaendelea kusema uwongo, akikaza kusema kwamba yeye ni Esau kweli. ***(Mwanzo 27:1-24)***<br>• Isaka akakula chakula ambacho Yakobo alimletea. Alipomaliza, akabariki Yakobo, akiwaza kwamba ni Esau. ***(Mwanzo 27:25-29)*** *Isaka atajisikia namna gani wakati atatambua kwamba walimudanganya?*<br>• *Unawaza, kwa nini Mungu alituamuru tusiseme uwongo?*<br>• *Mufikili Pamoja kuhusu mfano wa Bwana Yesu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Mwanzo 27:20***, **ao *Zaburi 32:2***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Mwana mpedwa wa Isaka alikuwa nani?<br>• Mwana mpendwa wa Rebeka alikuwa nani?<br>• Isaka alitaka kufanya nini kwa ajili ya Esau kabla ya kufa?<br>• Rebeka alipenda kwamba Esau apate baraka? Kwa nini?<br>• Yakobo na Rebeka walifanya namna gani kwa ajili ya kumudanganya Isaka?<br>• Kwa nini Isaka hakujue kwamba ilikuwa Yakobo kweli?<br>• Katika historia hii, unawaza kwamba Yakobo na Rebeka walimpendeza Mungu? Kwa nini? |

## A9 SOMO 3
**Yakobo anakutana na Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Tunaweza kumutumainia Mungu kwa sababu kila mara anatimiza ahadi zake.<br>• Mungu anatutunza.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ama Mwanzo 28:16, ao Zaburi 86:11***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 28:1-22*** |
| **KUTANGULIZA** | • Kumbukeni pamoja na watoto jinsi Yakobo alimudanganya Esau katika somo iliyotangulia. Esau alikasirika sana na alikuwa na nia ya kumuua Yakobo. Sasa Yakobo aliamua kuondoka nyumbani kwa muda.<br>• Ambia watoto wajiweke pahali pa Yakobo. Wangejisikia namna gani ikiwa wangeondoka nyumbani mu namna ile?<br>• Kuwaeleza kwamba, hata kama Yakobo alifanya vitu vibaya, Mungu alimuchunga kila mara na alimupenda. Katika mafundisho ya leo, tutaona jinsi Mungu alijionyesha kwa Yakobo. |
| **KUFUNDISHA** | • Isaka alibariki Yakobo, akimwambia aende katika familia ya mjomba yake Labani kule Padani-Aramu. Kule ilimpasa kupata mke na kumuoa. ***(Mwanzo 28:1-5)***<br>• Katika safari yake, Yakobo akasimama sababu ya usiku. Akatwaa jiwe moja akaitia chini ya kichwa chake. *Fikili kwanza!* Alipokuwa akilala, akaota ndoto. Akaona kipandio kimesimamishwa juu ya inchi, na kichwa chake kilifika mbinguni. Malaika za Mungu wakipanda na wakishuka juu yake. ***(Mwanzo 28:10-12)***<br>• Mungu akasimama juu ya kipandio. Akamwambia Yakobo kwamba atambariki na atampa uzao mwingi. Akaahidi Yakobo kwamba atakuwa naye. Siku moja, atamrudisha katika inchi ile. ***(Mwanzo 28:13-15)*** *Musemee kuhusu ahadi ni nini. Kila mara sisi tunatimiza ahadi zetu? Kwa nini? Fasilia Watoto kwamba kila mara Mungu anatimiza ahadi zake. Yeye ni mwenye nguvu yote na hasemi uwongo.*<br>• Wakati Yakobo ameamka, anatambua kwamba Mungu yuko pale. *Muzungumzie woga wa Yakobo wakati anatambua uwepo wa Mungu. Alifanya vitu nyingi ambavyo havimpendeze Mungu. Lakini hata vile, kila mara Mungu anamchunga!* Kisha akachukua jiwe ambayo mwanzo aliweka chini ya kichwa chake na akamwanga mafuta juu yake. Akaita jina la pahali pale Beteli. Yakobo akaahidi kwamba, kama Mungu ni Pamoja naye na anamrudisha kwa baba yake, sasa Bwana atakuwa Mungu wake. ***(Mwanzo 28:16-22)*** Yakobo bado anahitaji kujua kwamba Mungu anatimiza ahadi zake kila mara!<br>• *Sisi tuko kama Yakobo kwa sababu sisi pia, tunafanya vitu ambavyo hatupaswi. Mungu anatupenda, kila mtu kibinafsi, na anatuchunga, kama vile alifanya na Yakobo. Eleza kwamba alituma Mwana wake kufa msalabani kwa ajili yetu. Bwana Yesu ni kama "kipandio" kwa ajili ya kutukaribisha kwa Mungu na kutusaidia kufika mbinguni.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Matayo 28:16*, ao *Zaburi 86:11.*** Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Kwa nini ilimpasa Yakobo kuondoka nyumbani kwake?<br>• Yakobo aliweka kichwa juu ya nini?<br>• Yakobo aliona nini katika ndoto yake?<br>• Mungu alisema nini katika ndoto yake?<br>• Mungu alimchunga ingawa vitu vibaya ambavyo alifanya wakati wa zamani?<br>• Tunajua namna gani kwamba Mungu anatuchunga?<br>• Yakobo alifanya nini na jiwe lile?<br>• Bwana Yesu anafanana namna gani na jiwe lile? |

**A9 SOMO 4**
**Yakobo anapata mke**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yakobo, mdanganyifu, alidanganywa.<br>• Tunapaswa kufanyia wengine kile tunachotaka watutendee.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ama Mwanzo 29:28 , ao Wagalatia 6:7***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 29:1-30*** |
| **KUTANGULIZA** | • Umekwisha Kwenda kwa wa memba wa jamaa ambao haukuwajua mbele? Uliishi mambo hii namna gani? Ao eleza historia moja, kulingana na mambo ambayo uliishi, inayofanana na ile. Uwakumbushe watoto kwamba Yakobo aliend a kutembelea mjomba yake Labani kule Padani-Aramu.<br>• Onyesha watu wapya katika historia: Labani na binti zake, Lea na Rakeli.<br>• Katika somo hii, Yakobo anavumbua jinsi mtu anavyojisikia wakati anadanganywa na mtu mwingine? |
| **KUFUNDISHA** | • Yakobo alikuwa njiani akielekea Padani-Aramu. Mwisho wa safari yake, anakuta wachunga kondoo karibu na kisima. Alijua mjomba yake Labani. ***(Mwanzo 29:1-8)***<br>• Rakeli, binti wa Labani, akafika kwenye kisima na kondoo zake. Yakobo akamsaidia kuteka maji kwa ajili ya kondoo zake akiondoa jiwe kwenye mlango wa kisima. ***(Mwanzo 29:9-10)***<br>• Yakobo akajitambulisha kwa Rakeli. Akapiga mbio kupeleka Habari kwa baba yake. Labani akamwita Yakobo kukaa pamoja naye. ***(Mwanzo 29:11-14)*** *Jaribuni kufikiria mazungumzo yao!*<br>• Yakobo akaanza kumtumikia Labani. Anapaswa kutumika muda wa miaka saba ili Rakeli awe mke wake. Anapendelea kuifanya, kwa sababu anampenda Rakeli. ***(Mwanzo 29:15-20)***<br>• Lakini Labani anamdanganya Yakobo. Kuliko kumpa Rakeli, akampa Lea kuwa mke wake. ***(Mwanzo 29:21-27)*** *Yakobo alijisikia namna gani wakati alipotambua kwamba alidanganywa? Ambia Watoto wakumbushe namna Yakobo alidanganya watu wengine.*<br>• Yakobo akamuoa pia Rakeli lakini anapaswa kutumika miaka saba ya nyongeza. ***(Mwanzo 29:28-30)*** Inaonekana kwamba Labani alipata faida kwa Yakobo!<br>• *Unawaza kwamba Yakobo alihuzunika wakati ambao alidanganya wengine?*<br>• *Tunaweza kuwaza kwamba mwisho Yakobo amepata kile alichostahili. Muzungumzie kitu hiki Pamoja na Watoto.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, **ama *Mwanzo 29:28*, ao *Wagalatia 6:7***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Labani aliishi wapi?<br>• Ma binti wawili wa Labani waiitwa namna gani?<br>• Yakobo alimsaidia namna gani Rakeli wakati alifika kule Padani-Aramu?<br>• Yakobo alipenda binti gani kati ya hawa wawili?<br>• Yakobo alipendekeza kutumika muda wa miaka ngapi ili amuoe Rakeli?<br>• Labani alimdanganya Yakobo namna gani? |

## A10 SOMO 1
## Stefano anatoa Maisha yake kwa ajili ya Bwana Yesu

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Stefano alipenda Mungu na adui zake.<br>• Yesu alikuwa pamoja na Stefano wakati walikuwa wanampiga mawe na alikuwa anamuongojea mbinguni.<br><br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 4:19***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 6:8-15; 7:54-60*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwatie watoto moyo ili wazungumzie kuhusu wakati ambao walisaidia watu wengine.<br>• Wangewaza nini, ikiwa walitaka kusaidia mtu na yeye hapendi? Na hata alikuwa mkali kwao mu kiwango cha kutaka kuwatendea vibaya?<br>• Historia ya Biblia leo ni kuhusu mtu moja ambaye alikuwa anasaidia wengine. Lakini walifanya nini kwa hiyo? |
| **KUFUNDISHA** | • Stefano alimpenda Bwana Yesu. Alikuwa anafanya miujiza na alikuwa anasaidia watu, lakini Wayuda wengine hawakumpenda Stefano, wala Yesu. Kwa hiyo wakaamua kwa siri wamutendee mabaya na kumuzuiza kwambia watu kuhusu kufa kwa Yesu. ***(Matendo 6:8-11)***<br>• Watu hawa wakafunga shauri ya kumfanyia Stefano mashitaki ya uwongo na wakachochea watu. Wakamuleta mbele ya baraza ili waamue mambo yake. Wakaleta hata washuhuda wa uwongo juu ya Stefano. ***(Matendo 6:12-15)*** *Ungejisikia namna gani ikiwa wewe ulikuwa Stefano?*<br>• Ingawa uwongo kuhusu Yesu na kuhusu yeye mwenyewe, Stefano hakukasirika. Watu waliona kwamba Yesu alikuwa pamoja naye; wakaona kwamba uso wake ulikuwa kama wa Malaika. ***(Matendo 6:15)*** Stefano alimtetea Yesu lakini ile iliongeza tu hasira ya watu hawa. ***(Matendo 7:54)*** Kuliko kuogopa, Stefano akatazama mbinguni kule akamuona Yesu akimuongojea. ***(Matendo 7:55-56)*** *Stefano alijisikia namna gani wakati alimuona Yesu?*<br>• Watu walikasirika sana na hawakutaki kusikia chochote. Wakampeleka Stefano inje ya mji na wakamtupia mawe makubwa ili wamuue. Wakati walikuwa wanafanya vile, Stefano aliomba kwamba Yesu apokee roho yake na awasamehe watu hawa mabaya yote ambayo walikuwa wanamfanya. Kisha, akakufa. ***(Matendo 7:57-60)***<br>• *Kabla ya kufa, Stefano akamuomba Yesu afanye kitu moja kwa ajili ya adui zake. Unawaza, kwa nini alifanya vile?*<br>• *Tunaweza kusamehewa namna gani matendo mbaya yote ambayo tunatenda?*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***1 Yoane 4:19***. Eleza kwamba Stefano alionyesha mapendo yake kwa ajili ya Bwana Yesu kwa kuitika kufa juu yake. Bwana Yesu alikuwa amekwisha kuonyesha mapendo yake kwa ajili ya Stefano kwa kutoa uzima wake msalabani kwa ajili yake. |
| **KURUDIA** | • Stefano alikuwa msaada wa bei sana ndani ya Kanisa. Alikuwa anafanya nini?<br>• Watu wote walimpenda Stefano? Kwa nini?<br>• Wayuda walichochea watu namna gani?<br>• Stefano alifanya nini mbele ya uwongo ambao walisema juu yake na juu ya Yesu?<br>• Stefano aliona nini wakati alitazama mbingu?<br>• Watu walimfanya Stefano nini?<br>• Stefano aliomba nini katika maombi yake?<br>• Tunaweza kusamehewa namna gani? |

## A10 SOMO 2
**Filipo anahubiri Habari njema**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Tunapaswa kumwamini Bwana Yesu ili zambi zetu zisamehewe.<br>• Mungu anatusaidia kuelewa maandiko magumu katika Neno lake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 8:25***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 8:26-40*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uliza watoto jangwa iko inafanana na nini. Tunaweza kujisikia namna gani katika jangwa? Ikiwa umeombwa wende katika jangwa ili uzungumze na mgeni, utaenda kule?<br>• Ao, uliza watoto wakumbuke wakati fulani ambao walipata magumu kwa kuelewa kitu fulani, kwa mfano kitabu, ao shida la hesabu. Ni nani aliweza kuwasaidia? |
| **KUFUNDISHA** | • Filipo alimwamini Yesu na alikuwa anahubiri Habari njema yake katika eneo lote. Siku moja, Malaika akamwambia aende katika njia ya kusini, jangwani. *(Filipo aliwaza nini juu ya agizo hii?)* Eleza kwamba Filipo aliona gari ikikaribia. Inaonekana kwamba msafiri huyu ni mtu mwenye heshima wa Etiopia anayerudi kwake. *(Onyesha Etiopia iko wapi).* ***(Matendo 8:26-28****) Kulingana na wewe, huyu mtu wa Etiopia anasikia sasa hivi Habari ya nani?*<br>• Kisha, Roho Mtakatifu anamwambia Filipo ajongee karibu na gari hili. Mtu huyu alikuwa akisoma kwa sauti kubwa historia ya nabii Isaya, kitabu moja cha Agano la Kale. Filipo anamuuliza kama anaelewa vitu anavyosoma, lakini anajibu kwamba hapana. ***(Matendo 8:29-31)*** *Katika moja ya ma shairi, muna jambo la mtu ambaye ameuawa kama mwana kondoo. (Eleza kwamba mwana kondoo hasumbuki wakati anapelekwa kwenye machinjo.)* Filipo anaonyesha kwamba katika shairi hii ni kuhusu Bwana Yesu ambaye alikufa msalabani kwa ajili ya zambi zetu. *(Eleza kwamba Yesu alikuwa tayari kufa hivi).*<br>• Mtu huyu wa Etiopia anaelewa sasa kwamba amefanya zambi na anahitaji usamehe wa Mungu. Bila kusita, ametia Imani yake ndani ya Yesu Kristo, ambaye alikufa kwa ajili yake. ***(Matendo 8:32-35)***<br>• Kisha, Filipo alimbatiza kwa kuonyesha kwamba tangu sasa amekuwa mwanafunzi wa Yesu. *Fasilia ubatizo ni nini, kwa maneno iliyo rahisi). Eleza badiliko na furaha katika maisha ya mtu huyu.*<br>• Kisha Roho Mtakatifu alimnyanyua Filipo ili aende pahali pengine kutangaza habari ya Yesu. ***(Matendo 8:36-40)***<br>• *Mungu anataka wote wajue kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya zambi zao. Sema kuhusu wale wanaotusaidia kuelewa ujumbe wa Biblia. Tunapaswa kushukuru kwa sababu tumesikia habari njema kuhusu Yesu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 8:35***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Malaika alimtuma Filipo pahali gani?<br>• Mtu huyu alikuwa mtu wa inchi gani?<br>• Kwa sababu ya nini Filipo alimkaribia?<br>• Mtu huyu alikuwa anasoma nini?<br>• Alifanya nini wakati Filipo alimfasilia Habari njema ya Yesu?<br>• Alibatizwa wapi?<br>• Alijisikia namna gani alipoendelea na safari?<br>• Tunaweza kusamehewa zambi zetu namna gani? |

**A10 SOMO 3**
**Saulo na nuru inayoangaa**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu anapenda watu wote, hata wale wanaomchukia, naye alikufa kwa ajili yao, bila ubaguzi.<br>• Pekee yake Bwana Yesu ana nguvu ya kubadilisha Maisha yetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorinto 5:17***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:1-9*** |
| **KUTANGULIZA** | • Saulo alikuwa myuda ambaye alimchukia Yesu. Alichukia pia wote ambao walikuwa wanamfuata, mu kiwango cha kwamba alitaka kuwaona wote wafariki. Eleza kwamba alihuzuria kupigwa mawe kwa Stefano. (Somo 1).<br>• Uliza watoto kama wangetamani kwamba Saulo awe rafiki yao. Kwa nini? |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja, Saulo akaenda kule Damasiki, ili akamate wakristo na kuwaweka katika kifungo. ***(Matendo 9:1-2)*** *Muwaze pamoja kuhusu nia na matendo ya Saulo muda wa hii safari.*<br>• Alipokaribia Damasiki, gafula anaona nuru inaangaza ikimzunguka na anaanguka chini. *Tumia maneno ya Biblia ambayo ilisemwa kwa Saulo pia maneno yenyewe ya jibu lake. Eleza namna Saulo aliweza kujisikia wakati huu.* ***(Matendo 9:3-4)***<br>• Sauti inajibu: “Mimi ndimi Yesu”. *Eleza ni nini Saulo anaelewa mara moja: Yesu ni Mwana wa Mungu, yeye ni hai, mawazo ambayo alikuwa nayo juu yake ni ya uwongo!* Yesu anamwambia aingie katika mji wa Damasiki mule ataambiwa ambayo yanampasa kufanya. Watu ambao walisafiri pamoja na Saulo walishangaa, kwa sababu walisikia sauti lakini hawakuona mtu. ***(Matendo 9:5-7)***<br>• Wakati Saulo anasimama, haone kitu na inapaswa ashikwe mkononi kwa ajili ya kumuongoza katika Damasiki. Anabaki siku tatu pasipo kuona, bila kula kitu, wala kunywa. ***(Matendo 9:8-9)*** *Alijisikia namna gani wakati ambao alikuwa haone kitu?*<br>• *Muzungumzie kuhusu sababu juu ya ile Bwana Yesu alikutana na Saulo mu namna hii. Uwakumbushe watoto mu kiwango gani Saulo alimchukia Yesu na wanafunzi wake. Alitaka kuwaona wote wafariki. Lakini Yesu alimpenda na alitaka kwamba awe mwanafunzi wake hata kama hakustahili kitu hiki. Bwana Yesu alitaka kubadilisha maisha yake!*<br>• *Tunamhitaji Bwana Yesu. Yeye pekee anaweza kuondosha zambi zetu na kutupa uwezo wa kuishi maisha mpya.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***2 Wakorinto 5:17***, ambatanisha shairi hii na Maisha ya zamani ya Saulo. Ni “katika Kristo” tu ndiyo Maisha yetu inaweza kubadilika ili vitu vyote viwe vipya. |
| **KURUDIA** | • Paulo alisafiri Kwenda mji gani?<br>• Alienda kule kwa sababu ya nini?<br>• Aliona nini?<br>• Alisikia nini?<br>• Sauti ilimwambia nini?<br>• Saulo ametambua nini wakati anaelewa kwamba ni Yesu ambaye anasema naye?<br>• Saulo hakufanye nini muda wa siku tatu?<br>• Ni nani ambaye pekee yake anaweza kutupa nguvu ili tuishi Maisha mpya? |

## A10 SOMO 4
**Saulo anakuwa mtu mpya**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu anataka kutusaidia, na kwa hiyo anatuma watu kwetu, kwa wakati unaofaa.<br>• Kama vile Saulo, Mungu anabadilisha maisha ya watu leo na anawafanya kuwa wenye mafaa kwa ajili yake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 9:20***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:10-25*** |
| **KUTANGULIZA** | • Rudieni katika sehemu ya kwanza ya historia ya Saulo. Watoto wanakumbuka vile Saulo “wa zamani” alikuwa? Wakristo wa Damasiki walijisikia namna gani juu yake? (woga…)<br>• Ilimpasa Mungu awatayarishe ili wawe tayari kupokea Saulo mpya kama mmoja katika jamaa la Mungu. Tutajua ni kitu gani kilafanyika. |
| **KUFUNDISHA** | • Mungu anasema na Anania katika ndoto akimwambia aende kumtafuta saulo. ***(Matendo 9:10-12)*** *Unawaza kweli alitaka kwenda? Kwa nini?*<br>• Anania anaogopa kwamba Saulo anataka kumkamata ao hata kumuua. Mungu anamtia moyo kwa sababu alichagua Saulo kwa ajili ya kazi moja ya kipekee. Atamtangaza Mungu kwa wale ambao hawamjui bado. ***(Matendo 9:13-16)***<br>• Anania anatii na anaenda kumwona Saulo. Anamwita “ndugu yangu”. *(Eleza ni kwa nini wao ni ndugu.)* Anamwambia kwamba ni Bwana Yesu ambaye anamtuma. Anamwekea mikono Saulo na anaona. Amejazwa na Roho Mtakatifu. Kisha anabatizwa na wanampa chakula. ***(Matendo 9:17-19a)****. Saulo aliona namna gani huku kutembelewa na Anania?*<br>• Baada ya muda kidogo, Saulo anakusanyika pamoja na wanafunzi wengine wa Yesu kule Damasiki. Mara moja anaanza kuhubiri kuhusu Bwana Yesu. *Eleza mawazo ya wale ambao walimkuta Saulo katika Damasiki. Paulo si kama vile walifikili hata kidogo!*<br>• Wayuda ambao walisikia Habari ya mabadiliko ambayo ilifanyika katika Maisha ya Saulo, hawakutaki kabisa ujumbe anaohubiri. Wanafunga shauri ili wamuue. Saulo anapaswa kuondoka Damasiki akisaidiwa na wanafunzi ambao wanamshusha usiku kwenye ukuta katika kikapu. ***(Matendo 9:19-25)*** *Onyesha wazi mabadiliko ambayo ilifanyika katika maisha ya Saulo na mambo ambayo aliishi tangu alipomwamini Yesu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 9:20***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Mungu alisema na Anania namna gani?<br>• Kwa sababu ya nini Anania aliogopa kwenda kumwona Saulo?<br>• “Kazi”mpya ya Saulo ilikuwa nini?<br>• Ni nini ilifanyika katika macho ya Saulo wakati Anania alipomuwekea mikono?<br>• Ni zawadi gani ingine ambayo Saulo alipokea wakati alitembelewa na Anania?<br>• Saulo alianza mara moja kufanya nini?<br>• Kwa nini Saulo aliondoka kupitia kikapu?<br>• Maisha yetu inaweza kubadilishwa namna gani kama ile ya Saulo? |

**A11 SOMO 1**
**Paulo (Saulo) katika Antiokia**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Wale wanamwamini Yesu wanaitwa “wakristo”.<br>• Mungu ana matengenezo ya pekee kwa ajili yetu wakati tunamwamini; anataka kwamba tuwe wasaidizi wake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 11:26***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 11:19-20*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uliza watoto namna gani wanaweza kusaidia katika ma hali mbalimbali. Kwa mfano, unaweza kusaidia namna gani mwalimu yako mwanaume ao mwanamke? Ao utasaidia namna gani nyumbani ikiwa mama yako ni mgonjwa?<br>• Eleza kwamba katika historia ya leo, tutakuta watu wawili ambao walifanya pamoja kazi ya Mungu. |
| **KUFUNDISHA** | • Habari njema ya Yesu ilihubiriwa na kanisa la Mungu iliongezeka. Waamini wengine walikaa katika mji wa Antiokia. Pale, waliweza kuhubiri Habari njema kwa wale ambao bado walikuwa hawajaisikia na wengi walimwamini Bwana Yesu. ***(Matendo 11:19-21)***<br>• Habari ya hivi vitu vikubwa ambavyo vilifanyika katika Antiokia ilifika kwenye kanisa la Yerusalema. *Waamini walijisikia namna gani kwa hiyo? (furaha)* Wameamua kutuma kule mtu moja anayeitwa Barnaba ili apate habari zaidi. Anaenda katika Antiokia ambako anafurahi kwa kuona waamini wapya wengi. Barnaba anafanya yote iwezekanayo ili awafundishe na kuwatia moyo wabakie wenye kuambatana na Bwana. ***(Matendo 11:22-24)*** *Barnaba alikuwa mtu wa namna gani?*<br>• Barnaba amezidiwa na kazi kule Antiokia na anahitaji msaidizi. Mungu anafanya kwamba amkumbuke Saulo, ambaye alikutana naye miaka ya mbele. Baada ya kugeuka kwake, Saulo alirudi kule Tarso, mji kwenye alizaliwa. Barnaba anakwenda kule Tarso kwenye anamchukua Saulo hata Antiokia ili amsaidie katika kazi. ***(Matendo 11:25-26)***<br>• *Eleza kwamba Antiokia ilikuwa pahali pa muhimu kwa Saulo/Paulo kwa sababu ni pale alianza kazi yake kama misionary. Hiyo ilikuwa kazi ya pekee ambayo Mungu alitayarisha kwa ajili yake.* Saulo na Barnaba walifanya kule muda wa mwaka mzima, wakifundisha waamini. Wakati ule, wanafunzi wa Yesu Kristo waliitwa pale “wakristo” mara ya kwanza. ***(Matendo 11:26)***<br>• *Wakati tunatia imani yetu ndani ya Bwana Yesu, sisi pia, tunakuwa wakristo. Tunakuwa na jina namna moja pamoja naye! Mungu ana matengenezo ya pekee kwa ajili ya kila mristo, kama vile kwa Paulo. Anataka kwamba wakristo wawe wasaidizi wake.*<br>• *Inapaswa kufanya nini juu ya kuwa mkristo?*<br>• *Ikiwa sisi ni wakristo, Mungu anaweza kututumia namna gani?*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 11:26***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Kanisa iliongezeka katika mji gani?<br>• Ni nani ambaye alitumwa Antiokia kutoka kanisa la Yerusalema?<br>• Barnaba alifanya nini katika Antiokia?<br>• Barnaba alihitaji nini wepesi?<br>• Barnaba aliendा kumtafuta nani?<br>• Saulo na Barnaba walikaa muda gani katika Antiokia?<br>• Ni jina gani ilipewa kwa wale ambao walimwamini Yesu?<br>• Kwa kweli Paulo alitumikia nani? |

## A11 SOMO 2
**Paulo (Saulo) katika Kipuro**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Tunapaswa kufanya uchaguzi mzuri tukimtumainia Bwana Yesu.<br>• Tunapaswa kuwaambia wengine kuhusu Yesu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 28:19***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 13:1-12*** |
| **KUTANGULIZA** | • Panga watoto katika ma kundi ya watu wawili, ili wafikili pamoja kuhusu vitu nyingi ambavyo wanajua kuhusu Yesu.<br>• Uwaambie kwamba katika historia ya leo, tunavumbua Paulo (uwaonyeshe kwamba jina la Saulo, inakuwa Paulo katika shairi hii) Barnaba, na Marko ambao wanaambia wengine Habari ya Yesu. |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja, wakristo wa Antiokia wanakusanyika. Paulo na Barnaba wanaenda. Roho Mtakatifu anafunulia viongozi wengine kwamba Barnaba na Saulo wanapaswa kumfanyia Mungu kazi moja ya pekee. Baada ya kuombea neno hii, Barnaba, Saulo, na Marko (ao Yoane, kijana mwipwa wa Barnaba) wamesafiri Kwenda Kipuro. ***(Matendo 13:1-4)***<br>• Walipokuja, wanapita katika kisanga chote, wakihubiri. Katika Pafo, wanakuta mchawi anayemtumikia mtawala wa Kipuro. Huyu amesikia Habari ya Barnaba na Paulo na anataka kuwajua. Anataka kusikia Neno la Mungu, lakini Elema, mchawi, anajaribu kumuzuiza kuamini. ***(Matendo 13:5-8)***<br>• Paulo anajua kwamba mchawi huyu anaongozwa na Shetani. Alipojazwa na Roho Mtakatifu, Saulo anamkazia macho, akimwambia kwamba mambo anayofanya ni mbaya na kwamba Bwana atamfanya kuwa kipofu. Paulo anapokwisha kusema maneno haya, Elema anakuwa mara moja kipofu kweli na anageukia pande zote akitafuta mtu wa kumwongoza. ***(Matendo 13:9-11)****. Eleza kwamba ni mbaya kumpinga Bwana Yesu.*<br>• Mtawala anaona uwezo mkubwa wa Mungu na anamwamini Yesu. ***(Matendo 13:12)***<br>• *Paulo, Barnaba, Marko pia mtawala walifanya uchaguzi mzuri kwa kumwamini Yesu. Elema, alifanya uchaguzi mbaya. Yesu anapenda kwamba sisi pia tumwamini.*<br>• *Kwa nini ujumbe kuhusu Yesu ndio wa muhimu kabisa kuliko yote?*<br>• *Unajua mtu ambaye alienda pahali pengine kwa ajili ya kuwaambie wengine habari ya Yesu?*<br>• *Wewe, unaweza kuwaambia watu wengine namna gani Habari ya Yesu?*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matayo 28:19***. Eleza kwamba ni maneno ya Yesu kabla ya kurudi mbinguni. Matengenezo yake ilikuwa kwamba wote (“mataifa yote”) wasikie Habari njema na wamwamini. |
| **KURUDIA** | • Ni nani ambaye alituma Paulo na Barnaba ili wafanye kazi ya pekee?<br>• Ni nani alienda pamoja nao?<br>• Walitumia njia gani ya usafiri?<br>• Walienda katika kisanga gani?<br>• Walikuta nani katika Pafo?<br>• Ni nani alimwamini Yesu katika pafo?<br>• Ni nini ilimfikia mchawi?<br>• Ni nani alisema maneno iliyo katika mstari muhimu? |

**A11 SOMO 3**
**Paulo anakutana na Ludia**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yeyote anayemwamini Yesu ataokolewa.<br>• Tunaweza kuzungumza na Mungu kila pahali na juu ya kila kitu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 2:21***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 16:6-15*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto wakuelezee kuhusu safari mrefu ambayo walifanya. Ulienda wapi? Ilichukua muda gani? Uliona nani wakati ulifika?<br>• Eleza kwa watoto kwamba katika historia ya leo Paulo na marafiki zake wanasafiri. |
| **KUFUNDISHA** | • Paulo na marafiki zake wawili, Sila na Timoteo, walisafiri katika kilomita nyingi, wakipita katika inchi nyingi. Roho Mtakatifu alikuwa anawaonyesha kabisa ni wapi Mungu alitaka waende. Ingawa pahali, pale walikuwa wanasimama, kila mara palikuwa watu wengi ambao walihitaji kusikia kuhusu Bwana Yesu. ***(Matendo 16:6-8)***<br>• Mwisho, wamefika katika mji kwenye pwani. Usiku ule, Paulo anapata ndoto ya kipekee, ana ono ambamo mtu moja wa Makedonia anamsihi aende kuwasaidia. Paulo anajua kwamba ni Mungu ambaye anawaonyesha wazi ni wapi wataenda baadaye. ***(Matendo 16:9-10)*** *Eleza kwamba Mungu alitaka wakaaji wa pahali pale wasikie Habari ya Yesu na ndio maana alituma kule Paulo na marafiki zake. Mungu asiangalie pahali tunapoishi. Anataka kwamba watu wote wasikie habari yake.*<br>• Mara moja wanapata chombo ili waende kule. Kwa wepesi, wanafika katika mji kubwa unaoitwa Filipi. Siku ya sabato, Paulo na marafiki zake wanaenda inje ya mji, pembeni ya mto. Kule, wanakuta wanawake wakiomba. ***(Matendo 16:11-13)*** *Wanawake pembeni ya mto walikuwa wanaomba Mungu. Na sisi, ni wapi tunaweza kusema na Mungu? (Fasilia watoto kwamba tunaweza kusema naye pahali pote).*<br>• Mmoja wa wanawake hawa anaitwa Ludia. Ni mwenye kuuza zambarau nyekundu. Anaamini Mungu tangu zamani lakini bado kusikia habari ya Mwana wa Mungu, Bwana Yesu. Anasikia kwa usikilivu mambo yote ambayo Paulo anasema. Anajua ndani ya moyo wake kwamba mambo anayosikia ni kweli na anatia tumaini lake ndani ya Bwana Yesu. Anafurahi kwamba Paulo amekuja katika mji wake! ***(Matendo 16:14-15)*** Familia yake yote inaamini pia. Wote wanabatizwa na Ludia anamwita Paulo na marafiki zake wakae kwake.<br>• *Tunaweza kumwambia Mungu nini? (Ongojea Watoto walete Mawazo. Uwaambie kwamba tunaweza kuzungumza mambo yote na Mungu).*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 2:21***. Eleza kwamba kuita jina la Bwana inamaanisha kumuomba atuokoe katika zambi zetu. Ndio kitu Ludia alifanya katika historia hii. |
| **KURUDIA** | • Taja jina moja la marafiki za Paulo.<br>• Ni nani aliwaonyesha pahali Mungu alitaka waende?<br>• Ni nini ilifanyika katika ono ya Paulo?<br>• Paulo na marafiki zake walitumia njia gani ya usafiri wakati walienda katika Makedonia?<br>• Walikuta wanawake pahali gani?<br>• Walikuwa wanafanya nini?<br>• Ludia alikuwa na kazi gani?<br>• Ludia alifanya nini wakati alisikia Habari njema ya Yesu? |

## A11 SOMO 4
**Paulo na Sila katika kifungo**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Imetupasa kumwamini Bwana Yesu ili tuokolewe.<br>• Wakristo ni wenye furaha kwa sababu wana Yesu kama Mwokozi.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 16:31***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 16:16-34*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto waseme ni nini ambayo inawafurahisha.<br>• Uwaambie kwamba katika somo ya leo, kuna watu wenye furaha. Uwatie moyo wasikie vizuri ili wajue ni nani. |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja, wakati Paulo na Sila walikuwa katika Filipi, walisaidia kijana moja mtumwa. Jambo hili liliwafanya mabwana wa binti huyo kukasirika na walikokota Paulo na Sila hata sokoni. Walisema maneno ya uwongo juu yao. ***(Matendo 16:16-21)***<br>• Paulo na Sila walipigwa na kisha waliwatupa katika kifungo. Mlinzi alifunga miguu yao katika minyororo. ***(Matendo 16:22-24)*** *Unawaza kwamba Paulo na Sila walijisikia namna gani wakati ule?*<br>• Katikati ya usiku, wafungwa wengine wanasikia Paulo na Sila wakiomba na kuimba sifa za Mungu. ***(Matendo 16:25)***<br>• Gafula, imesikiwa kelele ingine. Vitu vyote vinatikisika na vinaanza kutetemeka. Milango inafunguka na minyororo inaanguka. Ni tetemeko la inchi! ***(Matendo 16:26)***<br>• Mlinzi ameamka katika usingizi. Anaona milango yote ya kifungo iko wazi. *Mawazo yake ya kwanza ilikuwa nini?* Paulo anamtuliza akimwambia kwamba wafungwa wote bado weko pale. ***(Matendo 16:27-28)***<br>• Mlinzi anamuuliza Paulo, anapaswa kufanya nini apate kuokolewa, kwa sababu anajua kwamba ni mwenye zambi. Paulo anamjibu: “Amini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokolewa”. Paulo na Sila wanamufasilia mlinzi na nyumba yake kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya zambi zao. Mlinzi anapeleka Paulo na Sila kwake, anasafisha vidonda vyao, na anawapa chakula. Usiku gani wa furaha kwa mlinzi na nyumba yake kwa sababu wote walimwamini Yesu. ***(Matendo 16:29-34).***<br>• *Ni nani alifurahi katika historia hii? Kwa nini? (Uwatie moyo watoto waseme kuhusu Paulo na Sila, vilevile kuhusu mlinzi na nyumba yake. Onyesha kwamba watu hawa walifurahi kwa sababu Yesu aliwaokoa).*<br>• *Uwasaidie watoto kuelewa kwamba tunahitaji kuokolewa katika zambi yetu. Tunapaswa kumwamini Yesu kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu na alikufa kwa ajili yetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 9:31***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Paulo na Sila walisaidia nani?<br>• Ni nini iliwafikia?<br>• Walikuwa wanafanya nini katikati ya usiku?<br>• Ni nini ilifanyika wakati walikuwa wanaimba?<br>• Kwa nini mlinzi aliogopa baada ya tetemeko la inchi?<br>• Ni swali gani ambayo alimuuliza Paulo na Sila?<br>• Walimpa jibu gani?<br>• Mlinzi alifanya nini usiku ule?<br>• Tunaweza kujifunza nini katika somo hii? |

**A12 SOMO 1**
**Zakaria na Elizabeti**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kwamba:<br>• Mungu anajibu maombi.<br>• Majibu yanakuja wakati wa Mungu, sio wetu.<br><br>Mstari muhimu: Luka 1:13<br>Usomaji wa Biblia: Luka 1:5-25</td></tr>
<tr><td>KUTANGULIZA</td><td>• Zungumza pamoja na watoto kuhusu familia zao, hasa kuhusu kuzaliwa kwa mtoto. Kila mara ni wakati wa furaha kubwa.<br>• Uwaambie watoto wawaze kuhusu kitu fulani ambacho wanataka kabisa. Kwa nini wanataka kitu fulani ao kingine? Katika historia hii, bibi na bwana hawa walitaka kabisa, siyo kitu fulani, lakini mtu… mtoto.</td></tr>
<tr><td>KUFUNDISHA</td><td>• Zakaria na Elizabeti walipenda sana kupata mtoto. Miaka ilipita, na marafiki zao wengi walikuwa na Watoto, lakini wao walikuwa pekee. Walijisikia namna gani? Zakaria na Elizabeti walikosa nini kwa upekee kwa sababu hawakuwe na mtoto? Acha watoto wajibu kulingana na mazingira ya tamaduni yao wenyewe. (Luka 1:5-7)<br>• Wakaamua kumuomba Mungu juu ya jambo hili. Wanajua vizuri kwamba Mungu anajibu maombi! (Luka 1:13) Onyesha kwamba tunaweza kuleta mambo yoyote kwa Bwana katika maombi.<br>• Mungu alisikia maombi yao. Anatuma Malaika kukutana na Zakaria wakati anapofanya kazi ndani ya hekalu. Zakaria alijisikia namna gani wakati aliona Malaika? Malaika anamwambia asiogope na kisha anamwambia Habari njema: Elizabeti atapata mtoto na jina lake itakuwa Yoane. (Luka 1:11-13)<br>• Zakaria haamini mambo anayosikia! Anawaza kwamba yeye na elizabeti ni wazee sana kwa kupata mtoto sasa. Malaika anamwambia kwamba, kwa sababu haamini ujumbe kutoka kwa Mungu, atakuwa bubu hata kuzaliwa kwa mtoto yao. (Luka 1:18-20)<br>• Tunaweza kujifunza mafundisho ya muhimu sana kwa Zakaria: Wakati tunaomba inapaswa kwamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.<br>• Muwaze pamoja kuhusu mambo fulani ya kuombea leo!<br><br>Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.</td></tr>
<tr><td>KUJIFUNZA</td><td>Kujifunza mstari muhimu, Luka 1:13 Kueleza maana yake ikiwa ni lazima.</td></tr>
<tr><td>KURUDIA</td><td>• Mke wa Zakaria alikuwa nani?<br>• Walitaka nini kuliko kila kitu?<br>• Zakaria na Elizabeti walielekeza maombi yao kwa nani?<br>• Ni nani ambaye alikuja kukutana na Zakaria katika hekalu?<br>• Zakaria alifanya nini kwa kumuona Malaika?<br>• Malaika alimpa ujumbe gani?<br>• Ni nini ilimfikia Zakaria sababu hakuamini ujumbe ule?<br>• Ni nini iliyo ya muhimu kufanya wakati tunapoomba?</td></tr>
</table>

## A12 SOMO 2
**Maria na Gabrieli**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Maria aliitika ujumbe wa Malaika hata kama ilionekana kwamba haiwezekane.<br>• Mungu anaweza kutimiza ile inaonekana kwamba haiwezekane.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:37***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Luka 1:26-38*** |
| **KUTANGULIZA** | • Rudieni pamoja katika historia ya somo la mwisho. Kutembelewa na Malaika anayetangazia Elizabeti na Zakaria kuzaliwa kwa mtoto. Baada ya muda mfupi, Mungu anatuma Malaika juu ya matembezi ingine ya kipekee. |
| **KUFUNDISHA** | • *Onyesha tofauti iliyo kati ya Elizabeti na Maria.* Huyu alikuwa binti tu, mwenye kuchumbiwa na mtu anayeitwa Yosefu. Aliishi kule Nazareti. Siku moja, anatembelewa na Malaika anayeitwa Gabrieli. ***(Luka 1:26-27)*** *Uwasaidie watoto kuelewa kwamba haikuwe kitu cha kawaida kuona malaika na haikuwe kitu cha kushangaza kama Maria aliogopa.*<br>• Lakini Malaika anamwambia asiogope. Anasikia kwa utulivu wakati Malaika Gabrieli anamtangazia kwamba atapata mwana. Maria haelewi vizuri; yeye hana mume! Malaika anamwambia kwamba ni Mungu, Roho Mtakatifu, ambaye atampa mtoto huyu wa kipekee. Ataita jina lake Yesu. ***(Luka 1:29-34)***<br>• Yesu atakuwa mkubwa kuliko wote. Atakuwa Mwana wa Mungu. Hakika ilikuwa magumu kuelewa, lakini Malaika anamwambia Maria kwamba Hapana neno lisilowezekana kwa Mungu. ***(Luka 1:35-37)***<br>• Maria aliamini ujumbe ambao alitoka kusikia. Alikuwa tayari kushiriki katika mpango kubwa wa Mungu anayetuma Mwana wake katika dunia. Kuzaliwa kwa Yesu itakuwa muujiza wa ajabu. ***(Luka 1:38)***<br>• *Umekwisha kupewa ahadi ambayo ulikuwa na magumu kuamini?*<br>• *Unawaza, kwa nini Maria aliamini ujumbe wa malaika? Mungu anapenda kwamba kila mmoja wetu amwamini kama vile Maria alifanya.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Luka 1:37***. Watoto wanaweza kuwaza kuhusu vitu vingine “visivyowezekana” ambavyo Mungu alifanya katika Biblia? Tumsifu kwa ukubwa wake! |
| **KURUDIA** | • Maria aliishi wapi?<br>• Mchumba wake alikuwa nani?<br>• Malaika ambaye alimtembelea maria jina lake ilikuwa nani?<br>• Kwa sababu ya nini Maria hakuelewe muzuri ujumbe wa malaika?<br>• Mtoto huyu atakuwa tofauti na wengine mu namna gani?<br>• Maria alifanya nini na ujumbe huu?<br>• Mu namna gani Maria ni mfano wa kuiga?<br>• Ni nini haiwezekane kwa Mungu? |

# A12 SOMO 3
## Kuzaliwa kwa Yoane

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu alitimiza ahadi yake kwa Zakaria na elizabeti.<br>• Mungu anatimiza ahadi zake kwetu pia.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:76***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Luka 1:57-80*** |
| **KUTANGULIZA** | • Fikirieni pamoja kutokuwa na uwezo wa kusema muda wa miezi nyingi. Uwakumbushe watoto kwamba ilimfikia Zakaria kwa sababu hakuamini ujumbe wa malaika.<br>• Uliza watoto wanajisikia namna gani wakati wa Noeli ao wakati wa kumbukumbu ya kuzaliwa wakati wanapokea zawadi ambayo waliongojea sana. Ile inasaidia kufikiria namna Zakaria na elizabeti walijisikia wakati mwana wao alizaliwa, kama vile Malaika alivyoahidi. Wakati gani wa furaha! |
| **KUFUNDISHA** | • Wakati mtoto alipozaliwa, jirani na jamaa wanataka kumwita Zakaria sawa baba yake. Elizabeti anawaambia kwamba ataitwa Yoane. ***(Luka 1:57-60)*** *Kwa nini Elizabeti alisema kwamba ataitwa Yoane?*<br>• Wakati wanamuuliza Zakaria jina la mtoto, anaandika: “Jina lake ni Yoane”. ***(Luka 1:62-63)***<br>• Mara moja, anaweza kusema tena. Zakaria anashukuru na kusifu Mungu. *Kwa nini Zakaria anafanya vile? Mungu alitimiza ahadi yake; amefurahi sana kwa sababu mwana wake amezaliwa; anajua kwamba kwa wepesi Mungu atatimiza vitu vingine vikubwa.* Wote wameshangaa sababu ya vitu ambavyo wanatoka kuona. ***(Luka 1:64-66).***<br>• Yoane alikuwa mtoto moja wa kipekee. *Kwa nini? Uwakumbushe watoto kwamba wazazi wake walimuongojea muda wa miaka nyingi, lakini, kitu kingine cha muhimu, atakuja kwa ajili ya kutayarisha kuja kwa Bwana Yesu.*<br>• *Kila mara Mungu anatimiza ahadi zake kwetu pia. Taja ahadi zingine za Mungu ndani ya Biblia.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Luka 1:76***. Eleza kwamba  mstari huu ni moja ya sifa ambazo Zakaria alitoa kwa Mungu. |
| **KURUDIA** | • Mume wa Elizabeti alikuwa nani ?<br>• Kwa nini alikuwa bubu ?<br>• Majirani walitaka kumpa mtoto jina gani ?<br>• Kwa nini Zakaria na Elizabeti walimwita kwa jina na Yoane ?<br>• Ni wakati gani Zakaria aliweza tena kusema ?<br>• Yoane alipaswa kufanya kazi gani ya kipekee ?<br><br>**Kazi ya mikono:** Watoto wanaweza kufanya tangazo ya kuzaliwa kwa Yoane. |

## A12 SOMO 4
**Kuzaliwa kwa Yesu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu ni Mwana wa Mungu ambaye alikuja kwa ajili ya kutuokoa.<br>• Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kumtuma Bwana Yesu kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa ajili yetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:7***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Luka 2:1-7*** |
| **KUTANGULIZA** | • Muzungumzie somo kuhusu matengezo ambayo wakati mwingine inabadilika wakati wa mwisho kabisa. Leta mfano ulio wa maana kwa watoto, ao kupitia mambo ambayo waliishi wao wenyewe, ao ile wewe uliishi.<br>• Eleza kwamba wakati ulikaribia ambao mtoto wa Maria alipaswa kuzaliwa. Ingekuwa rahisi huko Nazareti, kwenye Yosefu na Maria walikuwa wanaishi, lakini… |
| **KUFUNDISHA** | • Mfalme wa kiroma aliamuru kwamba kila mmoja katika watu, arudi kwenye pahali pake pa kuzaliwa, ili ajiandikishe kwa sababu ya hesabu. Kwa hiyo Yosefu na Maria walipaswa kusafiri hadi Betelehemu. ***(Luka 2:1-5)*** *Jaribuni kufikiria kuhusu urefu huu pamoja na watoto: Ilikuwa karibu kilomita 140, maana yake karibu kutembea siku ine. Jaribu kujiweka pahali pa Maria na Yosefu. (Kwa watoto wa kiwango 2, eleza kwamba Mungu alikuwa mwenye kupanga kwamba mtoto azaliwe kule Betelehemu.)*<br>• Walipofika, mji ulikuwa mwenye kujaa, na hawakupata pahali pa kulala usiku. Wakati ambao mtoto aliyeahidiwa ulipaswa kufika ulikaribia sana. Mwishowe, walipumzika katika nyumba ya wanyama. ***(Luka 2:6-7)***<br>• Baada ya kuzaliwa, Maria alimfunika mtoto katika nguo za kitoto na alimlalisha katika sanduku ya kulisha nyama. ***(Luka 2:6-7)*** *Kwa nini Yesu alifunikwa na kulalishwa katika sanduku ya kulisha nyama? Saidia watoto waelewe ukubwa wa mtoto huyu ambaye anazaliwa pahali pa unyenyekevu. Unaweza kuleta mfano moja wa kinyume hiki katika tamaduni yenu ninyi.*<br>• *Mtoto Yesu ni wa kipekee kabisa. Yeye ni Mwana wa Mungu. Alikuwa tayari kuacha mbinguni na kuzaliwa duniani kwa ajili ya kutuokoa katika zambi zetu.* ***(Matayo 1:21)***<br>• *Hatutaki kusahau kwamba huu ndiyo ujumbe kubwa wa Noeli, na tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kumtumwa Bwana Yesu kwa sababu ya mapendo yake kwetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Luka 2:7*** Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Mke wa Yosefu alikuwa nani?<br>• Maria na Yosefu waliishi wapi?<br>• Walisafiri hadi mji gani?<br>• Kwa nini Maria na Yosefu walijikuta kule Betelehemu?<br>• Kwa nini walipumzika katika pahali amabapo kwa kawaida paliwekwa kwa ajili ya Wanyama?<br>• Maria alimlalisha mtoto Yesu katika kitu gani?<br>• Ni nini ambayo ilimfanya Yesu kuwa wa kipekee?<br>• Kwa sababu ya nini sisi tunahitaji Mwokozi? |

## Mashauri kwa wakufunzi wa masomo

**KIWANGO 1:**
- Ukurasa moja (mbili katika vitabu) kwa wiki ambayo zaidi kuna kazi ya kupaka rangi na maneno kidogo ya kuandika.
- Pointi kumi zimewekwa kwa wiki, na kiwango cha juu cha pointi 40 kwa mwezi.
- Pointi mbili imewekwa kwa kila jibu inayofaa yenye kuandikwa na ma pointi inayobaki imewekwa juu ya kupakaa rangi. Yote pamoja inafanya kiwango cha ma pointi 10 kwa kila somo katika wiki.
- Ni kawaida kwamba watoto wanaojifunza masomo za kiwango 1 hawajue bado kusoma vema. Watahitaji msaada wa wazazi wao ao walimu.

**KIWANGO 2:**
- Ukurasa mbili (ine katika kitabu) kwa wiki.
- Historia ya Biblia inaelezwa katika somo. Watoto wanapaswa kupata maneno ya somo, kupaka rangi, kujaza mstari muhimu, na vivyo hivyo.
- Ma pointi 20 imewekwa kwa wiki, na kiwango cha juu cha ma pointi 80 kwa mwezi.

**NAMNA GANI KUREKEBISHA MASOMO?**

- Kuangalia kila ukurasa kwa kuchunguza majibu.
- Kuleta ma pointi kulingana na majibu.
- Kutumia kalamu ya rangi tofauti na ile mtoto alitumia.
- Ongeza, ikiwa ni lazima, jibu inayofaa na kurekebisha makosa ya herufi (lakini hiyo haiwezi kupunguza kiwango cha pointi).
- Kupatia ma pointi kidogo kwa jibu isiyo ya kutosha kabisa ao ya kipande.
- Kuhesabu jumla ya ma pointi kwa mwezi na kuiandika katika ukurasa wa mwisho, pa fasi iliyotayarishwa.

Ni ya muhimu kuwa mwema katika namna ya kupana ma pointi na kufanya yote iwezekanayo kwa kuwatia moyo watoto katika majifunzo yao ya Biblia. Usisite kusema neno ya kutia moyo, sifa, katika sanduku iliyopangwa kwa ajili ya ile ukiandika kwa mfano rangi ilipakwa mzuri, usafi wa kazi, ma pointi iliyopewa, uelewa mzuri wa mafundisho, vivyo hivyo. Ni ya muhimu kwa mtoto kuwa mwangalifu kweli ili a tofautishe maoni. Maswali, maoni, misemo ya kutia moyo inaamsha akili ya mtoto. Lakini, kama ni misemo hiyo hiyo inarudiwa mara kwa mara, kwa wepesi itapoteza bei yake.

**KIWANGO 1**
**Maoni kwa jumla:**
“Isabelle ninafurahi hivi unaanza masomo hii na ninatumaini kwamba itakupendeza. Kupakaa rangi kwako ni nzuri sana! je unaenda shule? Uniambie! Nitafurahi kupata habari yako.”
“Kazi nzuri Anderea. Rangi mzuri! Ilikuwa mgumu kwa kufanya? Ulisahau kidogo katika somo ya mwisho.”

**Maoni ya kiroho:**
“Vizuri, Sara! Yairo alipaswa kufurahi sana wakati Yesu alimsaidia.”
“Jibu mzuri sana! Historia ya kifo cha Yesu ni ya huzuni sana, lakini alifufuka. Hii ni habari njema!”

**KIWANGO 2**
**Maoni kwa jumla:**
“Kazi mzuri, kama vile kila mara, Joanna. Nina uhakika wa kwamba mwalimu wako shuleni anafurahi pia juu ya kazi yako!
“Ninaona kwamba ni sasa hivi kumbukumbu ya kuzaliwa kwako, Simoni. Ulitayarisha kitu gani cha kipekee? Kweli, siku iwe njema kwako!”
“Ulijikaza kabisa. Kuna makosa kidogo. Usisahau kusoma majibu yako kila mara.”

**Maoni ya kiroho:**
“Ninapenda sana jinsi ulimpakaa rangi mtoto Yesu rangi katika sanduku ya chakula. Mungu alionyesha mapendo yake kweli kwa kumtuma katika dunia, sivyo?
”Rangi zako ni nzuri! mambo ilikuwa mbaya kwa Zakaria sababu ya kutokuamini mambo ambayo Mungu alimwambia! Baadaye hakuwe tena na shaka ya neno la Mungu.”
“Ma jibu mzuri sana! Mtu aliyekuta filipo katika jangwa alirudi na furaha. Alisikia na kuamini habari njema ya Yesu.”

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Congo-Swahili SWC

06/2025